**Upungufu** wa ushahidi wamweka huru aliyehukumiwa miaka 30 jela makosa ya udhalilishaji kingono



UKURASA 4

**Mwanafunzi** afa kwa tuhuma za kichapo kutoka kwa walimu

UKURASA 4



Nipashe

TESA

Jumanne Julai 20, 2021

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 12

'Inzi ni uhakika wa utajiri kwa vijana wabunifu'

Ukurasa 13

Inacholenga TPDC, vituo binafsi (2)

Wazazi, walez... wataraji e haya wasipowaanda... mabinti kupevuka

ELIMU

NA CHRISTINA MWAKANGALE

Ufunguo wa utajiri kwa kufuga samaki huu hapa

ELIMU ya ufugaji samaki inatajwa kuwa muhimu hasa kwa vijana ambao baada ya kuhitimu kila mwaka wanaendelea kukosa ajira.

Kujiajiri kwenye samaki kunawezekana kwenye maeneo tofauti yaliyo na vyanzo vya asili vya maji yakiwamo maziwa, mito hata bahari na pia kwenye mabwawa ya kuchimba ufugaji unawezekana hata kufanyika nyumbani.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Ugani na Uvuvi, Idara ya Utafiti Mafunzo katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Anthony Dadu, anasema ufugaji wa samaki unaoanza na elimu huwa na manufaa makubwa ikiwamo kipato.

UKURASA 11

Jumanne Julai 20, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580647

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Kilio tozo miamala ya simu chasikika

**•NI** maelekezo ya Rais Samia, mawaziri kujadili hatima leo... *Endelea ukurasa 2*



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile (kulia), akizungumza na vyombo vya habari kuhusu masuala ya tozo za miamala ya simu jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

## Mbowe sasa atangaza msimamo mpya CHADEMA

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### MAOFISA TRA MBARONI TUHUMA DAWA KULEVYA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imewakamata maofisa wawili wa Mamlaka...

UKURASA WA 8

### CCM YAIBUKA KIDEDEA UCHAGUZI MDOGO KONDE

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeibuka na ushindi katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Konde Kisiwani Pemba...

## Shahidi adai Sabaya alivamia dukani

UKURASA 5

**MICHEZO** SIMBA YAJITABIRIA MAKUBWA KIGOMA UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (kushoto), akizungumza na wananchi wa kisiwa cha Maisome, kilichoko Wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza, akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa mradi wa umeme wa jua unaotekelezwa katika kisiwa hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kilio tozo miamala ya simu chasikika

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema serikali imesikia kilio na maoni ya wananchi kuhusu tozo mpya ya miamala ya simu.

Amewaomba wananchi wawe watulivu wakati jambo hilo linatafutiwa ufumbuzi. Aidha, alisema Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ameitisha kikao cha kujadili suala hilo ili kuona panapofaa kurekebisha.

Mwigulu alitoa kauli hiyo jana ikiwa ni siku 19 tangu kuanza kwa utekelezaji wa Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka 2021/2022 baada ya Bunge kupitisha Sheria ya Fedha iliyofanya marekebisho na kuruhusu kodi na tozo mbalimbali 22.

Kodi ya miamala ilianza rasmi Julai 15, mwaka huu na kusababisha kuibuka mjadala mjadala mkubwa kwenye mitandao ya kijamii, ujumbe mfupi na sauti mbalimbali za kueleza maumivu ya kodi hizo.

Kilio kikubwa kiko kwenye viwango vinavyotozwa huku mwananchi akikatwa fedha ya kampuni ya simu, kodi ya serikali na kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kiasi cha baadhi kuona bora kusafiri kupeleka fedha kwa muhusika kwa kuwa nauli ni ndogo zaidi.

Aidha, serikali ilitoa ufafanuzi wa kodi hiyo huku baadhi ya mawaziri wakiwaomba wananchi kukubali kufunga mkanda kwa ajili ya kujenga uchumi kwa kuwa fedha hizo zitaelekezwa kwenye barabara vijijini, shule na huduma za afya ambazo zinagusa wananchi wengi.

Mwigulu aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na vyombo vya habari akiambatana na Waziri wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Dk. Faustine Ndugulile.

"Kwa maaneo ambayo wananchi wametoa ushauri na kuelezea namna ambavyo jambo hili linawagusa, lakini pia tumepokea maeneo ambayo yanatakiwa kutoa elimu zaidi ili kujenga uelewa wa pamoja ikiwa ni pamoja na viwango vinavyokatwa kwa anayetuma na anayetoa, lakini kuhusu mantiki ya jambo lenyewe," alisema Mwigulu.

Alisema jambo la tozo za miamala linatekelezwa kupitia sheria iliyopitishwa na Bunge, lakini kuna kanuni za utekelezaji zinazomhusu yeye kama Waziri wa Fedha na Mipango na maeneo mengine yanahusu Wizara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, ambazo zitajadiliwa na kupatiwa ufumbuzi.

Alisema leo kutakuwa na kikao kilichoitishwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kujadili suala hilo na pia kutakuwa na kikao kingine cha mawaziri wa wizara zote kuchambua kwa kina suala hilo.

"Lakini Mheshimiwa Rais naye alishaguswa na jambo hili, amesikia maoni ya Watanzania wote na yeye ametolea maelekezo kwamba tuyafanyie kazi maoni hayo," alisema na kuendelea. "Nitoe rai kwa wananchi kuwa watulivu kwenye jambo hili tutaendelea kuelezea na kutoa ufafanuzi kwenye kila maeneo yanayohitaji ufafanuzi na tutachukua hatua kwenye maeneo ambayo yanahitaji kuchukuliwa hatua ili ujenzi wa taifa letu uweze kuendelea kama ambavyo wananchi wamekuwa na shauku kubwa kuona ujenzi wa Taifa letu unaendelea kwa ajili ya maendeleo ya nchi."

Hata hivyo, Dk. Mwigulu aliwaonya ambao wana nia mbaya ambao mara zote wanapenda kupotosha ama kubadili dhana ya maana halisi ya jambo ambavyo lilikuwa limekusudiwa na kuwataka wasifanye hivyo, kwani mambo haya yana maslahi mapana kwa nchi.

"Haya ni mambo ambayo ni ya kisheria, sheria za nchi zinatakiwa kuheshimiwa, ni mambo ambayo ni ya kikanuni na mambo yanayohitaji uelimishaji... tutaendelea kufafanua, lakini yale yanayotakiwa kufanyiwa kazi niwaahidi Watanzania tutaendelea kuyafanyiakazi kama ambavyo viongozi wetu wakuu wamesema," alisisitiza.

Alisema tayari aliwapa maelekezo wataalamu wa mifumo kuangalia vipengele vya Sheria ya Mifumo ya malipo Serikalini pamoja na Sheria ya Mawasiliano ya Mtandao (EPOCA) inayoelezea kuhusu masuala ya miamala kwa njia ya mtandao na kuja na mapendekezo yatakayosaidia kufikia muafaka wa jambo hilo.

Waziri Dk. Ndugulile alibainisha kuwa wizara yake pia ambayo inaguswa moja kwa moja na tozo hizo, imeendelea kupokea maoni na kuchakata taarifa mbalimbali tangu tozo hiyo ianzishwe na kumwahidi Waziri wa Fedha na Mipango kwamba atampa ushirikiano kuhakikisha kwamba maelekezo yaliyotolewa na viongozi yanatekelezwa.

Alirejea kutoa wito kwa Watanzania kuwa watulivu wakati jambo hilo linafanyiwa kazi na kusema kuwa serikali ni sikivu na itafikia muafaka mzuri.

## Mwalimu kizimbani tuhuma kupokea rushwa 600,000/-

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma, imemfikisha mahakamani Kaimu Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mafurungu wilayani Chamwino, Malisero Saveli (29), kwa tuhuma za kuomba rushwa ya Sh. 600,000 ili asimchukulie hatua mwanafunzi mtoro.

Saveli ambaye ni Kaimu Mtendaji wa Kijiji cha Ilangali wilayani humo, alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma kwa madai ya kutomchukulia hatua mwanafunzi wa darasa la nne.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Taasisi hiyo Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, mtuhumiwa huyo aliomba rushwa ya Sh.600,000 na kupokea Sh. 400,000 kutoka kwa mtoa taarifa ili asimchukulie hatua mwanafunzi huyo kwa kitendo cha utoro wa mtoto.

Kibwengo alisema kitendo cha mwalimu kudiriki kuomba na kupokea rushwa ni kwenda kinyume cha taaluma yake kwa kukwamisha elimu badala ya kuchochea elimu.

Alisema mtuhumiwa huyo amefunguliwa mashtaka mawili ya kushawishi na kupokea rushwa kinyume cha Kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 Marejeo ya 2019.

Mkuu huyo alisema elimu ni ufunguo wa maisha na serikali kila kukicha inasisitiza kuwekeza zaidi katika elimu ikiwamo kuimarisha mazingira ya utoaji elimu.

# Mbowe atangaza msimamo CHADEMA

**Na Richard Makore,** MWANZA

MWENYEKITI wa CHADEMA, Freeman Mbowe, ametoa msimamo wa chama hicho kuanza kufanya mikutano ya hadhara na makongamano ya kudai Katiba mpya nchi nzima.

Akizungumza jijini Mwanza jana, Mbowe alisema chama hicho kimekwazwa na uamuzi wa Jeshi la Polisi kuzuia kufanyika kwa kongamano la Katiba Mpya na kuwashikilia wafuasi wake ambao waliachiwa juzi. Aidha, aliweka msimamo wa chama hicho kuanzia sasa kuwa hawaweki dhamana kwa mfuasi au kiongozi wao yeyote atakayekamatwa na kwamba waendelee kuwapo magereza.

Msimamo wa Mbowe umekuja siku chache baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, alipozungumza na wahariri wa vyombo vya habari Ikulu, Dar es Salaam, na kusema suala la Katiba Mpya lisubiri kwanza asisimishe nchi kiuchumi, huku akisema mikutano inayoruhusiwa ni ya ndani pekee.

Jambo la tatu alilozungumzia Mbowe ni mahitaji ya Katiba mpya kwa wananchi bila kujali makundi yao.

"Jumatano hii (kesho) tunafanya mkutano mkubwa wa kudai Katiba na hiyo haitaishia hapo tu bali tutakwenda nchi nzima kwa kuwa ni haki yetu," alisema.

Akizungumzia viongozi 38 waliokamatwa jijini Mwanza mwishoni mwa wiki wakati wakijiandaa kuhudhuria kondamano la kudai Katiba, Mbowe alisema kwa sasa mwanachama ama kiongozi atakayekamatwa hawatamwekea dhamana polisi ama mahakamani.

Kwa mujibu wa Mbowe, wamemsubiri Rais Samia kutatua jambo hilo la kuondoa zuio la mikutano na makongamano ya vyama, lakini imeshindikana jambo linalowakosesha haki ya kikatiba.

**FEDHA ZA KESI**

Aidha, alisema licha ya wafuasi wa CHADEMA kushinda kesi Mahakama Kuu na kuamuliwa warejeshewe Sh. milioni 350 walizolipa kama faini katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, lakini hawajapewa chochote.

Mbowe alisema mahakama iliamuru serikali baada ya kushinda kesi Mahakama Kuu kuwarudishia fedha zao, lakini bado.

**TAHADHARI YA CORONA**

Mwenyekiti huyo alisema chama hicho hakiridhishwi na namna tahadhari dhidi ya corona inavyochukuliwa, jambo linalohatarisha maisha ya watu na kuitaka serikali kuongeza mbinu katika suala hilo.

Aidha, alisema hadi sasa hakuna bajeti yoyote iliyotengwa kwa ajili ya kushughulikia corona, huku akiainisha gharama za kumhudumia mgonjwa mmoja katika hospitali za kawaida kwa wiki ni zaidi ya Sh. milioni 2.5, huku hospitali za binafsi zinatoza mpaka Sh. milioni 15 kwa mgonjwa mmoja.

Alisema licha ya kuwa wananchi wengi ni maskini, lakini serikali haijasema mikakati maalum kwa ajili ya kuwasaidia ikiwamo kubeba gharama za matibabu.

## HABARI KITAIFA

# Upelelezi kesi ya Grace wakamilika

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limesema limekamilisha uchunguzi wa tukio la Grace Mushi (25), anayedaiwa kumfungia ndani ya nyumba aliyekuwa mpenzi wake na kuichoma moto, na kwamba wanatarajia kukabidhi jalada kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa ajili ya hatua zaidi.

Grace anatuhumiwa kumuua aliyekuwa mpenzi wake Khamis Abdallah (25), mkazi wa Mbezi Makabe, baada ya kudaiwa kumfungia ndani ya nyumba na kuimwagia mafuta ya petroli na kisha kuichoma moto.

Tukio hilo lilitokea Julai 16, mwaka huu saa 8:30 usiku.

Aidha, jeshi hilo limesema bado linamshikilia mtuhumiwa huyo na kwamba katika upelelezi wao wamebaini alihusika moja kwa moja katika mauaji hayo.

Kamanda wa Polisi Kanda hiyo, Muliro Jumanne, alisema jana kuwa:

"Katika tukio lililotokea Mbezi Makabe, maarufu kwa Mzungu, bado tunamshikilia mtuhumiwa kwa makosa ya mauaji na tumebaini kwamba kitendo cha yule binti kumfungia mwenzie kwenye nyumba, kutafuta petroli na kutafuta moto kuchoma nyumba ni vigezo vikubwa vitatu kwamba alifanya maandalizi ya kuua."

"Na vigezo hivi ndivyo vinatusukuma tuishawishi Ofisi ya Mashtaka itutolee mashtaka dhidi ya mtuhumiwa huyu, kile kitendo hakikubaliki na tunaona anastahili kufikishwa mbele ya sheria ili ajibu tuhuma zake."

### MAUAJI SINZA

Wakati huo huo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Ramadhani Kingai, akizungumza na Nipashe kwa simu, alisema hakuna mtuhumiwa linayemshikilia kuhusiana na tukio la mauaji lililotokea juzi katika hoteli ya Lemax iliyopo Sinza Dar es Salaam, baada ya mfanyabiashara Alex Koroso (37) kumuua kwa kumpiga risasi sita kijana Gifti Mushi, naye kujiua.

"Katika tukio lile la mauaji kwenye baa ya Lemax, hakuna kesi na hatuna mtu tunayemshikilia kwa sababu, aliyefanya tukio lile tayari ameshakufa, tunachofanya ni kukamilisha taratibu zetu za ndani za kufunga kesi," alisema Kingai.

Aliwataka wananchi kuwa na utaratibu wa kutoa taarifa kwa jeshi hilo pale wanapobaini kuna viashiria vya matumizi mabaya ya silaha kwa wale wanaomiliki.

"Kwa mfano tukio lile la juzi Sinza, mashuhuda walisema kwamba aliyefanya mauaji yale alikuwa ameanza kuonyesha ishara za matumizi yasiyo sahihi ya umiliki wa silaha hiyo, kwa hiyo walipaswa kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi na tungeweza kuchukua hatua haraka na kuzuia mauaji yale," alisema Kingai.

### SIFA ZA KUMILIKI SILAHA

Muliro, alisema sifa za mtu anayetakiwa kumiliki silaha ni lazima awe mwanadiplomasia, awe kwenye kampuni ya ulinzi au mtu mwenye akili timamu ya kutambua mazuri na mabaya.

Sifa ya pili alisema anatakiwa awe na kumbukumbu zinazomwonyesha kuwa na tabia njema huku sifa ya tatu akisema anatakiwa awe ni yule ambaye matendo yake yanafahamika kwenye jamii kabla na baada ya kumiliki silaha.

"Ndiyo maana kabla ya mtu kumilikishwa silaha, mamlaka husika zinazommilikisha zinatakiwa zione mihtasari ya kamati za ulinzi na usalama za kata, mtaa, wilaya, mkoa na baadaye taifa, ili kusaidia kuonyesha ni mtu wa aina gani anayemilikishwa na anastahili au laa," alisema Muliro.

"Na ikitokea umemilikishwa silaha, ukabadilika kitabia, sheria inarudi kwenye mistari ile ya sifa za kupoteza umiliki, na ukipatikana ushahidi wa kutosha kwamba umekiuka taratibu za umiliki, unaondolewa sifa za umiliki na inarudishwa kwenye mamlaka husika."

"Sheria inamtaka mtu aliyepewa silaha awe nayo wakati wote, sababu kwa mujibu wa sheria wakati mwingine unapoiacha nyumbani au kwenye gari ni tatizo," alisema.



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene (kushoto), akikagua baadhi ya nyumba za polisi katika kambi ya Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) ikiwa ni ziara ya kikazi iliyoanza jana mkoani Iringa. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

## Polisi: Disko toto marufuku Idd Dar

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limepiga marufuku 'Disko toto' katika kumbi zote za starehe, katika kipindi cha kusherehekea sikukuu ya Eid Al Adha inayotarajiwa kuadhimishwa kesho.

Sikukuu ya Eid El-Hajj huadhimishwa kila mwaka duniani na waumini wa dini ya Kiislamu na huadhimishwa kuanzia siku 10 tangu kuonekana kwa mwezi wa Dhu al-Hijjah kwa mujibu wa imani ya dini hiyo.

Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Muliro Jumanne, alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama limejipanga kikamilifu kuimarisha usalama katika kipindi hicho.

Pia aliwaasa wananchi wa eneo hilo na Watanzania kwa ujumla kusherehekea sikukuu hiyo kwa amani na utulivu, sambamba na kujiepusha na vitendo vya uvunjifu wa sheria.

"Jeshi la Polisi Kanda Maalum limejipanga kuimarisha doria maeneo yote muhimu zikiwamo nyumba za ibada, fukwe za bahari na kumbi za starehe na maeneo mengine yote yatakayokuwa na mikusanyiko mikubwa ya watu ili kuhakikisha wananchi wote wanasherehekea sikukuu hii kwa amani na utulivu.

"Pia wamiliki wa kumbi za starehe wanatakiwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa kumbi hizo," alisema Muliro.

Aliongeza kwa kuwataka wazazi kuhakikisha kuwa watoto wao hawatembei peke yao bila ya kuwa na uangalizi wa karibu na kutowaruhusu kuogelea peke yao ili wasizame na kupoteza maisha.

Aidha, madereva wa vyombo vya moto waendelee kufuata sheria za usalama barabarani ikiwa ni pamoja na kutoendesha magari au pikipiki wakiwa wametumia pombe/vilezi.

# Mil. 85/- za mikopo umiza zarejeshwa kwa wenyewe

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma imerejesha jumla ya Sh. milioni 85.4 ambazo wananchi walitapeliwa na watu au taasisi mbalimbali kinyume cha sheria.

Miongoni zipo Sh. milioni 12 za mwalimu mstaafu aliyekuwa amekopa Sh. milioni 3.3 kwa kampuni binafsi, lakini riba iliongezeka na kufikia kiasi hicho, na wahusika walichukua kadi yake na kuzitoa kwenye akaunti yake.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, watu mbalimbali walilalamika kudhulumiwa fedha zao ikawalazimu kufanya operesheni za kurudisha fedha hizo.

Taarifa hiyo ilisema zaidi ya Sh. milioni 44.2 kati ya milioni 55.5 zilirejeshwa kwa wakulima waliokuwa wameporwa na vyama vya msingi, baada ya wakulima kuuza mazao kwa mfumo wa stakabadhi ghalani kisha watumishi baadhi wasio waaminifu kutoka katika vyama hivyo kuwadhulumu fedha hizo.

"Pia Sh. milioni 12 zilirudishwa kati ya milioni 96 alizodhulumiwa mwalimu mstaafu Yusuph Bakari, aliyekopa jumla ya Sh. milioni 3.3 kwa watu wawili binafsi na taasisi moja ya ukopeshaji fedha.

"Pensheni yake ya Sh. milioni 96 ilipoingia kwenye akaunti yake, wafanyabiashara hao wawili na taasisi moja ya ukopeshaji fedha walimteka na kumleta mjini, wakafanya (connection) benki moja (jina limehifadhiwa) na kumpora Sh. milioni 63 na baadaye kwa kutumia kadi yake, kampuni ya ukopeshaji ikachukua Sh. milioni 33 kwa nyakati tofauti," alisema Mtatiro.

Aidha, taarifa hiyo ilibainisha kuwa hayo yalitokea kati ya Februari 14 hadi 18 mwaka 2019.

Ilisema mwalimu huyo aliripoti Polisi, lakini hakupata ushirikiano kwa wakati. Miaka miwili baadaye Julai 2021 alimfikishia suala hilo Mkuu wa Wilaya ya Tunduru na ndipo alichukua hatua, na fedha zake zimeanza kurejeshwa baada ya waliomuibia kukiri kuwa walimdhulumu. Mtatiro pia alirejesha Sh. milioni 18.3 kwa wanachama wa (Tunduru Teachers Saccos), baada ya kutapeliwa na viongozi wao, pia fedha hizo ni asilimia 15 ya fedha zote wanazopaswa kulipwa.

"Tunaendelea na kazi ya kusimamia hadi wote walipwe fedha zote. Pia Sh. milioni 10.8 zilirejeshwa kwa wananchi wengine mbalimbali na taasisi za kukopesha pesa na watu binafsi," alisema.

## Maofisa TRA mbaroni tuhuma dawa za kulevya

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imewakamata maofisa wawili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), pamoja na aliyekuwa askari polisi wakidaiwa kuwa na dawa za kulevya jijini Dar es Salaam.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Gerald Kusaya, aliwataja maofisa wa TRA waliokamatwa ni Andrew Paul (45), pamoja na Ally Juma (32), pamoja na aliyekuwa askari polisi mwenye namba F 6763 Deodatus Massare.

Kamishna Kusaya alisema Juni 21, mwaka huu katika maeneo ya Mivinjeni Wilaya ya Temeke, vyombo vya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na maofisa wa DCEA walimkamata ofisa wa TRA, Andrew Paul, akiwa na wenzake wawili wakiwa na dawa za kulevya aina ya heroin kilo 1.02.

"Ofisa huyo alikuwa na wenzake ambao ni Said Mgoha maarufu kama Kindimu kazi yake ufundi gereji, George Mwakang'ata, mfanyabiashara wakiwa na kiasi hicho cha dawa," alisema Kusaya.

Alisema Juni 23, mwaka huu maofisa wa DCEA na vyombo vya ulinzi na usalama walimkatama ofisa mwingine wa TRA , Ally Juma, akiwa na Abubakar Abdallah ambaye ni mfanyabiashara wakiwa na dawa za kulevya aina ya Methamphetamine yenye uzito wa gramu 597.61.

Kamishna Kusaya alisema: "Katika upekuzi tulioufanya nyumbani kwa ofisa huyo wa TRA maeneo ya Zimbili Kinyerezi, kulipatikana Sh. milioni 82.043, pamoja na Dola za Marekani 5,100." Kadhalika, Kamishna huyo alisema Juni 19, mwaka huu katika eneo la Bunju jijini Dar es Salaam maofisa wa DCEA walimkamata aliyekuwa askari polisi, Deodatus Massare akiwa na dawa za kulevya aina ya heroin kilo 1.04.

Alisema Juni 18, mwaka huu katika eneo la Mburahati Madoto Wilaya ya Ilala maofisa wa DCEA waliwakamata mume na mke ambao ni Jamal Mangatule (45), na Mariyamu Bacha (28), wakiwa na dawa za kulevya aina ya heroin gramu 494.52.

Kamishna Kusaya alisema: "Watuhumiwa wote wameshafikishwa mahakamani wakikabiliwa na makosa ya kijihusisha na usafirishaji na biashara ya dawa za kulevya, makosa ambayo ni uhujumu uchumi. Bado tunaendelea na uchunguzi ili kuwabaini wahalifu wengine walioshiriki katika tukio hilo."

Aidha, Kamishna Kusaya alisema wameanza mapambano ya kukabiliana na wafanyabiashara wa dawa za kulevya, lengo likiwa ni kumaliza mtandao huo. Alisema katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Mei hadi Julai, mwaka huu DCEA wamefanikiwa kukamata kilo 953 za dawa za kulevya, huku Juni pekee zikikamatwa kilo 99.33.



Mtaalamu wa maabara wa Chuo Kikuu cha Hubert Kairuki (HKMU), Walter Msangi, akimweleza Mkuu wa Chuo hicho, Anne Makinda, kuhusu shughuli zinazofanywa na maabara hiyo katika kufundisha wanafunzi wa chuo hicho, ikiwa ni ziara yake chuoni hapo jana. Anayefuata ni Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Charles Mgone, Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Taaluma, Profesa Moshi Ntabaye na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, John Ulanga. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mwanafunzi afariki kwa kichapo cha kufeli mtihani wa 'Mock'

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

MWANAFUNZI wa Shule ya Sekondari wilayani Namtumbo, Mkoa wa Ruvuma mwenye umri wa miaka 15 (jina limehifadhiwa), amefariki dunia kwa madai ya kupewa adhabu ya kipigo na walimu wake baada ya kufanya vibaya mitihani ya Mock mkoa.

Mwanafunzi huyo ni miongoni mwa watu wengine watatu waliopoteza maisha wilayani humo katika matukio tofauti.

Kamanda wa Polisi mkoani Ruvuma, Joseph Konyo, akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, alisema katika tukio la kwanza Jeshi la Polisi linafanya uchunguzi wa kifo cha mwanafunzi huyo ambaye inadaiwa Julai 18, mwaka huu majira ya saa 3:00 asubuhi katika kituo cha Polisi cha Namtumbo kilipokea taarifa za kifo chake.

Alisema inadaiwa katika taarifa hiyo mwanafunzi huyo alifariki wakati akipatiwa matibabu Kituo cha Afya cha Hanga baada ya kulazwa kutokana na majeraha ya kupewa adhabu ya kuchapwa viboko yeye pamoja na wanafunzi wenzake wa kidato cha kwanza na cha tatu.

Alisema inadaiwa Julai 19, mwaka huu, majira ya saa 5:00 asubuhi mwanafunzi huyo akiwa na wenzake walipewa adhabu na walimu wao kwa kufanya vibaya kwenye matokeo ya Mock mkoa walioufanya kabla ya kufungwa shule.

Alisema inadaiwa baada ya adhabu hiyo mwanafunzi huyo aliumia na kupata uvimbe kwenye paja la upande wa kulia pia katikati ya mgongo na ndipo wazazi wake walipompeleka Kituo cha Afya Hanga na siku ya pili majira ya saa 10:00 jioni mwanafunzi huyo alifariki dunia wakati akiendelea kupatiwa matibabu.

Kamanda Konyo alisema, walimu sita wa Shule ya Sekondari Mbunga wanashikiliwa na polisi kwa mahojiano zaidi.

Alilitaja tukio lingine la Julai 17, mwaka huu majira ya saa 7:00 mchana katika Kijiji cha Marungu, Kata ya Tingi, wilayani Nyasa, mwanaume mmoja mwenye umri wa miaka 85 (jina limehifadhiwa) mkazi wa Kijiji cha Marungu aliuawa baada ya kuvamiwa nyumbani kwake kisha kukatwa na shoka kichwani na mtu asiye fahamika.

Inadaiwa kabla ya tukio hilo mwanaume huyo alikuwa amelala nyumbani kwake na mkewe mwenye umri wa miaka 84.

Kamanda alisema, alikuja mtu na kuanza kugonga mlango kwa nguvu kama anabisha hodi bila kusema chochote ndipo mwanaume huyo alipolazimika kuamka na alipofungua mlango alivutwa nyuma ya nyumba yake na kuangushwa chini kisha mtuhumiwa akaingia ndani na kuchukua shoka lililokuwa sebuleni ambalo alilitumia kumkata kichwani na kumsababishia kifo mzee huyo ambaye inadaiwa alikuwa akilalamikiwa kwa imani za kishirikiana.

Polisi inaendelea kumsaka mtuhumiwa wa tukio hilo.

Katika tukio la tatu inadaiwa Julai 17, mwaka huu, majira ya saa 4:00 usiku katika Kijiji cha Lugali, Kata ya Mkumbi, wilayani Mbinga, mwanaume mwenye umri wa miaka 40 mkazi wa Kijiji cha Ngima wilayani humo, aliuawa na watu waliojichukulia sheria mkononi kwa kumkata miguu na mwili kwa kutumia kitu chenye ncha kali wakimtuhumu kuwa ni mwizi wa kuku.

Katika tukio hilo polisi inamshikilia mtuhumiwa mmoja na msako wa kuwakamata wahusika wengine unaendelea.

Pia, katika tukio lingine Julai 18, mwaka huu majira ya saa 2:00 usiku katika Kijiji cha Mtumbati Maji, Kata ya Mgombasi, mwanaume mmoja mwenye umri wa miaka 25, mkazi wa kijiji hicho alikutwa akiwa amefariki kwenye tembe la kuchomea tumbaku.

Alifafanua zaidi kuwa inadaiwa mwanaume huyo alikuwa ameenda shambani Julai 17, mwaka huu, kukagua maendeleo ya uunguaji wa tumbaku yake na alikuwa anaichoma na ndipo alipopatwa na ajali ya kuangukia kwenye shimo la tumbaku na kufia humo baada ya kuvuta hewa ya ukaa (carbon monoxide).

Kamanda Konyo alitoa rai kwa wananchi wanaojichukulia sheria mkononi kuacha mara moja.

# Upungufu wamfutia kesi aliyehukumiwa miaka 30 jela

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani imeainisha upungufu saba wa ushahidi wa Jamhuri katika kesi ya Majaliwa Ihemo, aliyekuwa akidaiwa kumwingilia kinyume cha maumbile mpenzi wake na kuamuru kufuta adhabu ya miaka 30 jela na fidia ya Sh. 1,500,000.

Uamuzi huo wa jopo la majaji watatu, Jaji Rehema Mkuye, Barke Sahel na Jaji Galeba ulitolewa baada ya kupitia rufani iliyokatwa na Majaliwa akipinga kutiwa hatiani na kuhukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30, jela na kulipa fidia ya Sh. milioni 1.5. Majaliwa alitiwa hatiani na Mahakama ya Wilaya ya Kibondo mwaka 2018 kwa makosa matatu, kubaka, kumdhalilisha na kumwingilia kinyume cha maumbile aliyedaiwa kuwa mpenzi wake.

Alikata rufani Mahakama Kuu Kigoma mbele ya Jaji Athumani Matuma, ambaye alifuta kosa la kubaka na udhalilishaji aliyofungwa miaka 30 na kuliacha kosa la kumwingilia kinyume cha maumbile ambalo alihukumiwa jela miaka 30, kosa ambalo alikatia rufani katika Mahakama ya Rufani akiwa na sababu tatu.

Mrufani anadaiwa kumlazimisha kufanya mapenzi na mpenzi wake, kumdhalilisha kwa kumwingizia chupa ya bia sehemu za siri na kumwingilia kinyume cha maumbile wakiwa nyumbani.

Katika sababu zake anadai Mahakama ilikosea kumtia hatiani na kumpa adhabu kwa manufaa ya mlalamikiwa wakati kesi haikuthibitika.

Anadai kosa la kumwingilia kinyume cha maumbile halijathibitika na Mahakama ilikosea kuegemea kwenye ushahidi wa kielektroniki wakati haukupokelewa kama kielelezo.

Baada ya kusikiliza hoja hizo na hoja za Wakili wa Jamhuri, Antie Julius anayedai mashtaka yalithibika bila kuacha shaka, Mahakama ya Rufani iliona kwamba ushahidi wa Jamhuri una shaka, hivyo iliainisha mashaka hayo.

# Shahidi adai Sabaya alivamia duka lake

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MASHAHIDI wawili katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya (pichani) na wenzake wawili ya unyang'anyi wa kutumia silaha, wameanza kutoa ushahidi wao jana kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha.

Shahidi wa kwanza Mohamed Saad (45) ambaye ni mfanyabiashara na mmiliki wa duka katika Mtaa wa Bondeni, jijini Arusha, alidai mahakamani hapo kuwa Ole Sabaya, Silvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38), walivamia duka lake ambalo alimwachia ndugu yake kumsaidia kuuza na kujifanya maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Akihojiwa na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Abdalah Chavula, Saada alidai mahakamani kuwa Februari 31, hadi Aprili mwaka huu, alimwachia ndugu yake, Numan Jasini (ambaye ni shahidi wa pili katika kesi hiyo), kumsaidia kuuza duka.

Alidai Februari 9, mwaka huu, majira ya saa 11 jioni, alikwenda kwa fundi sofa aliyetambulika kwa jina la Hussein, na baada ya muda alipigiwa simu na Numan, kwamba kuna wateja walitaka kununua bidhaa dukani kwake, lakini walitaka kuhudumiwa na mwenye duka.

Alidai baada ya muda mfupi kupita mmoja wa wateja alimpigia simu kuzungumza naye akimtaka kufika dukani kwake, lakini alimweleza kwamba yupo mbali hivyo hawezi kwenda.



"Baada ya kukataa kwenda muda si mrefu mmoja wa wateja hao, alimnyang'anya Numan simu yake na kunipigia akaniambia nakupa dakika tano uwe umefika hapa, niliendelea kumsisitiza kwamba nipo mbali sitoweza kwenda."

"Wakati wakiendelea na majibizano hapo dukani, nilipigiwa tena simu na Numan, akiniambia kwamba hao ni maofisa kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wanamwitaji dukani."

"Ndugu yangu Numan wakati akizungumza na mimi nilisikia kwenye simu wakimwambia kwamba wao ni maofisa kutoka TRA, na wanahitaji nifike kwenye duka langu la biashara haraka ndani ya dakika tano."

Shahidi huyo alidai alimpigia simu ndugu yake mwingine Ali Saad na kumwambia aende kuwasikiliza maofisa hao wa TRA, na alipofika alimpigia simu kumweleza kwamba aliyekuwapo ni Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na wenzake.

"Nilimuuliza ndugu yangu, huyo mtu anataka nini? Alinijibu huyu DC wa Hai ana tabia ya kuwasumbua wafanyabiashara hivyo nikapiga simu kwa ndugu yangu mwingine, Hajirin Saad, afike dukani kwa kuwa kuna maofisa wa serikali wamefika hapo."

"Baada ya muda kidogo Hajirin, alinipigia simu, kuwa kuna watu kama maofisa wa TRA, wapo dukani hapo na nilisikia mabishano makali kwenye simu na nilipokata simu nilichukua usafiri wa pikipiki kwenda msikiti wa Kijinge kwa sababu nilikuwa na hofu, hivyo niliona sehemu hiyo ndiyo salama kwa wakati huo."

Alidai kuwa alipofika msikitini aliwapigia simu ndugu zake wote, hawakupatikana na alikaa msikitini hadi majira ya mbili usiku.

"Baada ya sala ya saa mbili usiku nilichukua usafiri wa pikipiki kwenda kwa rafiki yangu, Said Mohamed, kwa jina maarufu Samoki, anaishi eneo la makaburi ya Baniani, Kata ya Ngarenaro."

"Nilipofika kwa rafiki yangu nilipiga simu nyumbani kwangu, nikaambiwa kuna watu wanavunja mlango wa nyumba yangu, ilikuwa majira ya saa tatu usiku, hivyo nikampigia simu jirani yangu anaitwa Abui, hakupokea simu."

"Nilikuchua hatua ya kumpigia simu jirani mwingine anaitwa kwa jina maarufu Dokta, ni mtoto wa Ibrahimu Mvungi, nilimuomba aniangalizie hapo nyumbani kwangu, na alinieleza kwamba amewaona watu wanavunja mlango wakiwa na magari matatu ya serikali yenye namba za UN."

Alidai baada ya majibu hayo, alimpigia simu mke wake, na alimweleza kwamba wameingia nyumbani kwao wakiwa na silaha aina ya bastola, na walifanya upekuzi nyumba nzima na waliwatishia kwamba waseme alipokuwa Mohamed.

"Nipoambiwa hivyo, nilikaa kwa Samoki hadi alfajiri ya siku iliyofuata kwa kuwa walisema hadi wanipate, na baada ya muda nilipiga simu kwa ndugu yangu, Ali Saada, nilimpata, aliniambia kwamba wana hofu sana kwa kuwa kuna magari yamepaki tena kwenye nyumba ya mama yao wakisubiria kama kuna mtu atatoka ndani."

Alidai Februari 17, mwaka huu, aliporudi kutoka mafichoni (porini), wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, alibaini kiasi cha Sh. 2,769,000, ziliibiwa dukani kwake.

"Kwa kuwa nilimwachia Numan duka, aliniambia kiasi hicho cha fedha kiliibiwa na watu hao walipokwenda dukani," alidai.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**
**"INSTITUTE OF CONSTRUCTION TECHNOLOGY (ICoT)"**

**TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'**

**1. Utangulizi:**
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Chuo cha Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi chenye makao yake makuu katika Manispaa ya Morogoro. Chuo kinawatangazia wananchi wote kuwa kinatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo / Changarawe kwa kutumia Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi katika vituo vilivyopangwa kama ifuatavyo:-

| | Jina la kozi | Tarehe ya kuanza na kumaliza mafunzo | Mahali Mafunzo yatakapo fanyika |
|---|---|---|---|
| | | | |
| 1. | Kozi ya uwekaji wa tabaka la Lami kwenye barabara za miji na vijiji ('Bituminous surfacing of low traffic volume roads') kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Nne (4)** **30/08/2021 - 24/09/2021** | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya)** |
| 2. | Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi.(Kozi Na.26) | **Wiki Kumi (10)** 04/10/2021 – 10/12/2021 | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya)** |

**2. Masomo yatakayofundishwa: -**
(a) Kozi ya ukarabati na matengenezo ya Barabara za Udongo / Changarawe: Washiriki watajifunza mambo mbali mbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi.Pia, watajifunza mambo mbali mbali juu ya: mpango wa kazi (Planning), Uongozi sehemu za kazi na mbinu za usimamiaji wa kazi, vipimo vya kazi, usimamiaji wa mikataba, Uwekaji wa tabaka la changarawe pamoja na ujenzi wa makalavati. Kozi hii imekusudia kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kutosha katika kufanya na kusimamia kazi za ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe / udongo kwa ubora wa hali ya juu.

**3. Njia za ufundishaji**
Mafunzo yatafanyika KATIKA AWAMU MBILI; awamu ya kwanza itakuwa nadharia (darasani) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo.

**4. Malengo ya kozi**
Masomo katika kozi hizi yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali juu ya matumizi ya Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:
i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Reccurent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani "SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS" kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinayotolewa na TARURA au TANROADS.

**5. Walengwa wa Mafunzo haya ni:-**
a) Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo / ukarabati wa barabara kwa kutumia Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. Lugha ya mafunzo:-**
**Lugha itakayo tumika kufundishia katika kozi zote ni kiingereza.**

**7. Gharama za Mafunzo:-**
**Gharama za mafunzo zitakuwa kama ifuatavyo:**

| JINA LA KOZI | MUDA (Wiki) | ADA (TSH.) |
|---|---|---|
| Kozi ya uwekaji wa tabaka la Lami kwenye barabara za miji na vijiji ('Bituminous surfacing of low traffic volume roads') kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | Nne (4) | 1,000,000/= |
| Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | Kumi (10) | 1,600,000/= |

Ada ya ushiriki zilipwe kwa kutumia 'control number' itakayotolewa kwa mtu yeyote atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

**8. Namna ya Kutuma Maombi ya Kozi hizi:-**
Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi yoyote kati ya hizi zilizotajwa hapo juu wanatakiwa kutuma maombi yao Chuoni ICoT, tawi la Mbeya kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

Kumbuka: Kuna nafasi za malazi ishirini (20) tu kwa kila kozi; hivyo, inashauriwa kutuma maombi mapema iwezekanavyo.

**Wasiliana nasi**

**Mkuu wa Chuo**
**IcoT- Mbeya**
**Wilaya ya Rungwe**
**S.L.P 1957, MBEYA.**

**Simu : 025 295 7484/5; 0787 059 555; 0769 317 404; 0765 251 509**
**Nukushi : 025 295 7486**
**Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com**

216364602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaomilikishwa silaha waangaliwe afya ya akili

**JULAI** 17, mwaka huu, eneo la Sinza, jijini Dar es Salaam, kulifanyika mauaji ya kutisha baada ya mfanyabiashara Alex Koroso (37), kumshambulia kijana mwenzake Gift Mushi, kwa risasi wakati wakiwa wanapata kinywaji.

Inadaiwa mfanyabiashara huyo alianzia baa nyingine alikokesha usiku kucha na baadaye kuhamia kwenye baa hiyo akiendelea kunywa na kutokea mabishano na wenzake.

Mabishano hayo yalisababisha mauaji hayo ambayo yamekuwa gumzo kutokana na matumizi mabaya ya silaha.

Tukio hilo limeshtua wengi na kuwa gumzo kwenye mitandao ya kijamii. Wapo wanaouliza kama wanaomilikishwa bastola wanapimwa akili na kuangaliwa mienendo yao kabla ya kupewa.

Wenye baa nao wameingia kwenye lawama kutokana na kutodhibiti watu wanaoingia na silaha wakiwa wamelewa kupita kiasi huku wakifanya vurugu kutoripotiwa polisi.

Video zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha awali, alivyokuwa anafundishwa kutumia bastola hiyo na pia Juni 13, mwaka huu, wakati wa kumbukumbu ya siku yake ya kuzaliwa moja ya keki ilikuwa na picha ya bastola yake.

Tukio hili linaamsha hisia na kuonyesha umuhimu wa kupitia upya utaratibu wa kummilikisha mtu silaha, na usalama kwenye maeneo ya starehe.

Kama marehemu Alex alianza kurusha risasi hewani wakati anapishana na wenzake huku akimwaga risasi mezani, ilikuwa ni ishara tosha ya kutoweka kwa amani, ilipaswa waliokuwapo kutoa taarifa polisi kwa siri.

Upo umuhimu wa kupitia upya mienendo ya wanaomiliki silaha, lakini uwapo utaratibu wa kupima akili za wenye silaha hizo mara kwa mara bila kusubiri matukio ya mauaji, kama inavyotokea kwenye nchi zilizoendelea duniani.

Kwa uchache, Mei 11, mwaka huu, mtu mmoja nchini Urusi, aliua wanafunzi kadhaa kwa kuwafyatulia risasi wakiwa shuleni kwenye mji wa Kazan.

Juni 20, mwaka huu, watu 12 waliuawa kwa kupigwa risasi na wengine 40 kujeruhiwa baada ya kupigwa risasi wakati wanatazama filamu mjini Denver nchini Marekani.

Mwaka 2017 waumini 26 wa Kanisa la First Baptist Church mji wa Sutherland Springs moja ya Jimbo la Texas waliuawa kwa kupigwa risasi wakiwa kanisani na kijana aliyekadiriwa kuwa na miaka 20.

Haya ni matukio ya mfano kwenye nchi zilizoendelea ambazo kumiliki silaha ni jambo la kawaida na zinauzwa maduka maalum, hata kijana wa miaka 20 anaweza kununua, na mauaji mengi nchini humo hutokana na kupigwa risasi.

Ni muhimu kujifunza kwa kuhakikisha ukaguzi unafanyika maeneo yenye mikusanyiko ya watu wengi kama uwanja wa taifa ambapo wengine hushindwa kujizuia dhidi ya utani wa mashabiki, wanaweza kufanya jambo baya (ingawa hatuombi litokee).

Kwenye maeneo mengine ya mikusanyiko ni muhimu kuimarisha ukaguzi, ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza na kuelimisha jamii umuhimu wa kutoa taarifa.

Wapo wanaomiliki silaha na kuona ni sifa kuzionyesha wakati mwingine kuvaa nguo za kubana zikionyesha silaha husika kiunoni, na wengine wanapokwenda sehemu za starehe wanazitoa na kuweka mezani au kuonyesha wengine jambo ambalo huchukuliwa rahisi, lakini ni hatari kwa usalama wa watu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Poleni mabinti, sheria sasa ichukue mkondo

**JUMLA** ya watoto 981, wamepata mimba katika kipindi cha miezi sita kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu, katika Wilaya ya Kibondo mkoani Kigoma, hali inayoonyesha kuwa jitihada zaidi za kupambana na unyanyanyasi watoto kingono zinahitajika.

Kwa hesabu hiyo, ni kwamba kila mwezi, watoto 163 wamepata mimba katika kipindi hicho wilayani humo, na kama ikitokea wilaya zote za mkoa zina tatizo hilo, maana yake ni kwamba idadi 'itatisha' na mabinti hawatasoma watakuwa wanalea.

Akiwa katika ziara Kibondo, yenye lengo la kukagua na kujionea utoaji wa huduma za ustawi wa jamii na masuala ya maendeleo ya jamii, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, anaagiza watuhumiwa watafutwe na kuchukuliwa hatua.

Anataja mimba hizo kwa watoto kama kitendo cha ukatili wa kijinsi, na kwamba taarifa hizo haziwezi kufumbiwa macho, badala yake watendaji wanaohusika wafanye kila linalowezekana ili watuhumiwa wapatikane na haki inatendeka katika kipindi kifupi.

Kimsingi, jamii haiwezi kutegemea miujiza ya mafanikio ya kizazi kijacho iwapo itabaki kufumbia macho vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto kwa kuangalia watoto wao wakidhalilishwa kingono katika umri mdogo, kuambukizwa maradhi, wengine kufariki kwenye uzazi na kupata ulemavu ikiwamo fistula wakati wa kujifungua.

Hivyo kama anavyosema kiongozi huyo, ni vyema kila mzazi na mlezi kufanya sehemu yake katika malezi ya mtoto ikiwamo kumwepusha na mazingira yanayoweza kumsababishia kupata mimba za utotoni.

Wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao hudaiwa kushirikiana na watu wanaowapa mimba mabinti kwa kumalizakana kimya kimya, inawezekana mazingira kama hayo ndiyo yamefanyika hata katika wilaya ya Kibondo, kwa kuwa hakuna hatua zilizochukuliwa hadi serikali ilipotoa maelekezo ya kukamatwa watuhumiwa.

Hivyo ili kumaliza tatizo hilo, mabadiliko yanatakiwa kufanyika kuanzia kwa wazazi na walezi, watambue umuhimu wa elimu kwa watoto wao na kuachana na tamaa ya kutaka mali kwa njia zisizo halali.

Watoto wa kike wanatakiwa kuachwa waendelee na masomo yao bila ya usumbufu, hivyo wazazi na walezi wanaoshiriki kuwaoza, watambue kuwa wanawaharibia ndoto zao kielimu na hata afya.

Katika kutokomeza mimba na ndoa za utotoni, ni vyema nguvu ziendelee kuelekezwa katika uwekezaji kwenye elimu kwa watoto wa kike, wawe shuleni, wasome bila vikwazo.

Hatua hiyo inaweza kubadilisha mitazamo kuhusu majukumu ya kijinsia na usawa wa kijinsia na kutambua kuwa mtoto wa kike ana haki ya kupata elimu kama ilivyo kwa mtoto wa kiume.

Mbali na hilo, suala la elimu ya afya ya uzazi inatiliwa mkazo kwa watoto waliofikia kuvunja umri wa ungo, ili kuzuia mimba na pia kuhimiza wazazi na walezi waweze kushiriki kikamilifu katika vita dhidi ya ndoa na mimba hizo.

Kila upande ukitimiza wajibu, ni rahisi kutambua kuwa mimba za utotoni huathiri afya, elimu na haki za mtoto wa kike, kwa kuwa mtoto wa kike asiye na elimu itamuwia vigumu kupata maisha bora na kujitegemea baadaye.

Kadhalika binti anayepata mimba akiwa na umri wa miaka 14 au pungufu inaelezwa kuwa haki zake zinakiukwa, hivyo ili awe salama, ni muhimu wadau wote kushiriki katika vita dhidi ya mimba na ndoa za utotoni.

Pamoja na mbinu na njia mbalimbali ambazo zinatumika kudhibiti mimba za utotoni tatizo limeendelea kuwapo kama hilo la Kibondo, hali inayoashiria kuwa kuna haja ya kuchukua hatua zaidi.

# CCM yaibuka kidedea uchaguzi mdogo Konde

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeibuka na ushindi katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Konde Kisiwani Pemba, uliofanyika kwenye vituo 16 vya jimbo hilo na mgombea wa chama hicho, Sheha Mpemba Faki, akichaguliwa kwa kura 1,796.

Kwa majibu wa matokeo yaliotangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi Tume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC) Jimbo la Konde, Yassin Jabu Khamis, katika kituo cha majumuisho ya ya kura, Micheweni mgombea kutoka Chama cha ACT-Wazalendo, alipata kura 1,375.

Vyama vingine ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kura 857, CUF (624), Ada-Tadea (56), Demokrasia Makini (56), NCCR-Mageuzi (83), TLP (45), SAU (39) na TLP kura 45.

Kadhalika vyama vingine ikiwamo UPDP kilipata kura 29, NRA (44) na CKK (18), kati ya wapigakura waliojiandikisha kupiga kura katika jimbo hilo ambao ni 6,636 huku waliojitokeza kupiga kura ni 5,050 na zilizoharibika ni 30.

Mbunge mteule wa jimbo hilo, Sheha Mpemba Faki aliwashukuru wapigakura kwa kumpigia kura kuwa mbunge wa jimbo hilo.

Alisema atajitahidi kutekeleza yale yote ambayo aliahidi katika kampeni za uchaguzi mdogo alipokuwa akipita kuomba huku akiwapongeza viongozi mbalimbali wa CCM kwa kumuunga mkono katika mbio hizo.

"Nawaahidi wananchi wa Jimbo la Konde sitowaangusha nawaomba tuendelee kushirikiana kwa ajili ya kuleta maendeleo ndani ya jimbo letu," alisema.

Mwenyekiti wa CUF Wilaya ya Micheweni Pemba, Mbwana Haji Mbwana, alieleza kuwa uchaguzi ulikuwa wa amani na utulivu, ijapokuwa chama chake kilishatoa tamko kwamba hakitoshiriki uchaguzi hadi itakapopatikana katiba mpya na tume huru ya Uchaguzi.

Mbwana alidai kwamba mgombea wa chama hicho, Salama Khamis Kombo katika uchaguzi mdogo wa jimbo la Konde na aliyepata kura 624, alishiriki bila ya idhini ya CUF.

Mwenyekiti huyo alidai kuwa alikubaliwa na NEC kugombea nafasi hiyo kwa Chama cha CUF, ingawa kulikuwa na vigezo vya kukubalika na muhuri wa chama pamoja na kuwekwa saini.

"NEC ilimkubali mgombe huyu kuwa ni miongoni mwa wagombea kutoka CUF kutokana ndani ya Fomu yake kuwa na vigezo ikiwamo muhuri, Mwenyekiti wa Chama Wilaya ndio mwenye muhuri na sijalifanya hilo la kumuwekea muhuri, saini," alisema.

Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Wilaya ya Micheweni, Rashid Khalid Salim, alisema kuwa matokeo wameyapokea ingawaje hawakuridhika nayo kutokana na kuwapo baadhi ya dosari ndogo ndogo ambazo waliona huenda zitajitokeza tena. "Sisi tumeyapokea matokeo kama yalivyotolewa na tume ingawaje hatukufurahi moja kwa moja kutokana na dosari zilizojitokeza ambazo kila mara wakati wa uchaguzi tunazieleza, ikiwamo kunyimwa karatasi za matokeo na jimsi ya uhesabu wa kura," alieleza mwenyekiti huyo.

# Tanzania, Rwanda kushirikiana sekta ya TEHAMA

**Na Hellen Mwango**

TANZANIA na Rwanda, zimekubaliana kuendelea kuwa washirika imara katika biashara na mawasiliano pamoja na kubadilishana teknolojia na mafunzo katika sekta ya mawasiliano.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Waziri Kindamba, alisema jana jijini Dar es Salaam wakati Waziri wa TEHAMA na Ubunifu wa Rwanda, Paula Ingabire, alipotembelea shirika hilo kwa ajili ya kuendelea kuunganisha uhusiano.

"Shirika hili linafanya kazi na Shirika la Mawasiliano la Rwanda kwa zaidi ya miaka 10 ikiwamo kuwezesha uwezo wa upatikanaji wa intaneti nchini humo.

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano nchini Rwanda imepiga hatua kubwa na tutaendelea kushirikiana katika nyanja mbalimbali, ili kuhakikisha sekta hiyo inaimarika na kushiriki katika kukuza uchumi wa nchi," alisema Kindamba.

Naye Waziri wa Rwanda, Ingabire alisema ziara yake inalenga kuona ushirikiano wa nchi hizo unavyoweza kuendelea kwa kuwa ni wa msingi katika kuendeleza nyanja mbalimbali.

Alisema, watajadili sekta binafsi za nchi hizo zinavyoweza kufanya kazi kwa pamoja na kuendelea kukuza uchumi wa nchi husika na kuimarisha maendeleo.

Alisema ipo haja ya kuwa na mfumo wa kubadilishana uzoefu baina ya wataalamu wa nchi husika kama uti wa mgongo wa kukuza uchumi wa nchi hizo ikiwa ni pamoja na kutumia mifumo ya kusoma kwa njia ya mitandao.

Alisema ipo haja kwa sekta ya mawasiliano, kufikia wakati kuwa kusaidia sekta nyingine kukua na kukuza uchumi wa nchi.

Kwa upande wake, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia, Dk. Faustine Ndugulile, alisema nchi ya Rwanda imekuwa na mabadiliko makubwa hasa katika sekta ya mawasiliano, jambo ambalo wanahitaji kuendelea kushirikiana.

Alisema ziara ya waziri huyo inalenga kufika katika kituo cha taifa cha data pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ili kuangalia ni wapi wataboresha zaidi ushirikiano wao kwa kuwa wamekuwa na mapinduzi makubwa kwa sekta ya mawasiliano na TEHAMA pia.


IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
AT KISUTU

~~RM~~/CIVIL/~~MISC~~/~~PRO~~/EMPL/~~MATR~~ CASE No. 96 OF 2018

THE CONTRACTORS REGISTRATION BOARD ........ PLAINTIFF

*Versus*

M/S RANKY INFRASTRUCTURE & ENGINEERING LTD. ........ DEFENDANT

NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION/JUDGMENT/RULING

TAKE NOTICE that, the above mentioned case has been fixed for ~~hearing~~/~~mention~~/judgment/~~ruling~~ on the 10th day of AUGUST 2021
At 7.00 PM

YOU are required to appear in this Court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to relay in support of your case.

GIVEN under my HAND and the SEAL of the Court this 13th day of JULY 2021.

PRINCIPAL/SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KISUTU – D'SALAAM

TO BE SERVED UPON:

MANAGING DIRECTOR
M/S RANKY INFRASTRUCTURE
& ENGINEERING LTD
P.O. BOX 46006
DAR-ES-SALAAM

216365602

## Wazazi wafundwa kuhusu watoto ufaulu duni sekondari

**Na Mary Geofrey**

WAZAZI wameshauriwa kutowakatisha tamaa wanafunzi walioshindwa kufanya vizuri katika elimu ya sekondari, badala yake wawatafutie njia mbadala ya kuendelea na elimu.

Wito huo, ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mwasisi wa Shule Huria ya Ukonga Skillfull, Tabaro Diodorus, wakati akiwapongeza wanafunzi 31 waliofaulu elimu ya kidato cha sita shuleni.

Alisema ni vizuri mwanafunzi akapewa nafasi ya kurudia mtihani badala ya kumkatisha tamaa na kumuona kuwa hataweza kufaulu tena.

"Wazazi na jamii tusiwahukumu watoto kwa kushindwa kufaulu elimu ya sekondari, tuwape nafasi ya kujirekebisha walipokosea.

Usimwambie kuwa atafeli kwa sababu hawa tunawapongeza leo hawakufanya vizuri katika matokeo yao ya kidato cha nne lakini leo hii wamefanya vizuri na wote 31 wanakwenda chuo kikuu," alisema Diodorus.

Alisema asilimia kubwa ya wanafunzi alionao wengi wao walifeli na wengine kuacha shule, wamewafundisha namna ya kujitambua na hatimaye wamefanya vizuri katika masomo yao.

Aidha, Diodorus alisema shule yake imejiwekea mikakati ya kuhakikisha wanaondoa daraja la nne na sifuri na tayari mpango huo umeanza kuzaa matunda katika matokeo ya kidato cha sita.

"Tunapompokea mwanafunzi jambo la kwanza tunataka kujua tatizo la mwanafunzi ambalo lilimfanya asifaulu mtihani na baada ya hapo tunaanza kufanyia kazi kile ambacho ametueleza na mwalimu wake ataanza kumfuatilia kwa ukaribu hiyo ni moja ya mikakati yetu katika kuhakikisha mwanafunzi anafanya vizuri katika mitihani yake," alisema.

Diodorus alisema shule yao imeweza kufanikiwa katika hilo na kuhakikisha wanaweka vipindi maalum ikiwamo kuwakutanisha na wataalamu wa masuala ya saikolojia.

Diodorus alisema wana amini kila mwanafunzi anauwezo wa kufaulu na endapo hajafaulu inategemea na wapi alipopita katika kupata elimu.

# Waziri aibukia kanisani kuhimiza kodi ya ardhi

**Na Munir Shemweta,** SONGWE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameibuka katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mwambani katika kata ya Mkwajuni wilayani Songwe na kuwahimiza waumini kuhakikisha wanalipa kodi ya pango la ardhi.

Akizungumza na waumini hao Jumapili, akiwa katika ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi kwenye mkoa wa Songwe, Dk. Mabula alisema, wamiliki wote wa ardhi nchini wanapaswa kulipa kodi ya pango la ardhi ili kuongeza mapato na kuiwezesha serikali kuwatumikia wananchi katika shughuli za maendeleo.

Aliwaeleza kuwa, ardhi ni mali na mtaji na katika kuitunza lazima iongezwe thamani kwa kupangwa, kupimwa na kumilikishwa.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, ardhi inaweza kutumiwa na wamiliki wake katika shughuli za maendeleo sambamba na kupunguza migogoro ya ardhi hasa ile ya mipaka na kusisitiza kuwa mmiliki anapaswa kuwa na hati ili kuwa na usalama wa miliki yake.

"Ukiwa na ardhi iliyopimwa utapunguza migogoro ya mipaka na majirani zako, usikae na ardhi bila kuipima, watu wanaongezeka kila siku ila ardhi haiongezeki na ninyi mmejaliwa kuwa na madini na kama una ardhi hakikisha una hati itakuja kukusaidia hapo baadaye," alisema Dk. Mabula.

Alisema wizara yake imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kuhakikisha migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali inakwisha, na kubainisha kuwa moja ya jitihada hizo ni uanzishwaji wa ofisi za ardhi za mikoa ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

Naibu Waziri Mabula amemaliza ziara yake katika mkoa wa Songwe ambapo mbali na kusikiliza na kuitafutia ufumbuzi migogoro ya ardhi katika mkoa huo alizindua Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya katika Mkoa wa Songwe.



Kazi ya ujenzi wa barabara ya Mwananyamala mkoani Dar es Salaam ikiwa inaendelea katika eneo hilo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kiwanda cha mbolea Morocco chamvutia Mkenda

**Na Mwandishi Wetu,** MOROCCO

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, ametembelea na kufanya mazungumzo na uongozi wa kiwanda cha kutengeneza mbolea cha 'Open Compute Project Foundation' (OCP) kilichoko nchini Morocco na kuridhishwa na ubora wa bidhaa zinazotengenezwa.

Akiwa ameambatana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Japhet Justine, Waziri Mkenda alijionea jinsi kiwanda hicho kinavyozalisha mbolea bora kwa ustawi wa mazao.

Akizungumza baada ya kutembelea kiwanda hicho, Prof. Mkenda mbali ya kufurahishwa na teknolojia, aliupongeza uongozi wa kiwanda hicho kwa kufanya mapinduzi katika sekta ya mbolea na kushika namba moja kwa uzalishaji bora wa mbolea duniani kwa mwaka 2020.

"Leo nimetembelea kiwanda hiki cha OCP kujionea wanavyofanya kazi kwa ubora wa hali ya juu na kwa dhati kabisa ningependa kuwapongeza kwa hatua waliyofikia kwa kutoka kukamata namba nne (4) kwa ubora hadi kufikia namba moja duniani mwaka 2020," alisema Prof. Mkenda.

OCP kinamilikiwa kwa ushirikiano ambapo asilimia 50 inamilikiwa na serikali ya Morocco na asilimia 50 zinazobaki zinamilikiwa na nchi za India, Pakistan, Ujerumani, Brazil na Ubelgiji na kutoa mchango mkubwa.

Prof. Mkenda aliuomba uongozi huo kuangalia uwezekano wa kutatua tatizo la kupanda kwa mbolea kukuzia mazao duniani jambo ambalo litaleta tija kwa kwenye sekta ya kilimo.

"Moja ya jambo la msingi nililojadiliana nao ni kuona namna gani mzuri ya wao wanaweza kwakatusaidia kupunguza gharama za mbolea kwa maana kwa kufanya hivyo tutakua tunamgusa moja kwa moja mkulima na kuleta tija katika sekta hii."

Prof. Mkenda ameongeza kuwa ziara hiyo imekua sehemu ya ushirikiano wa nchi mbili na sehemu ya mkakati wa serikali katika kuboresha mazingira ya sekta ya kilimo Tanzania.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Justine alielezea ziara hiyo kama moja ya ziara ya kujifunza na yenye kuleta matumaini chanya kwa maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.

Waziri Mkenda na Justine walikwenda Morocco wakati wa ziara ya kikazi wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

# Watumishi afya wapewa angalizo wizi wa dawa

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigella, amewataka wataalamu wa afya mkoani humo kuacha tabia ya kuiba dawa na kuuza kwenye maduka ya watu binafsi.

Shigella amesema vitendo hivyo ni kinyume cha taratibu za utumishi na ni kosa kisheria.

Shigella alitoa agizo hilo katika mkutano wa nusu mwaka wa tathmini ya mkataba wa lishe na Bima ya Afya ya Jamii (iCHF), na kwamba hivi karibu vimeripotiwa vitendo vya wizi wa dawa katika wilaya za Kilombero na Mvomero.

Amesema kuna haja ya kuimarisha mfumo wa utoaji dawa kwa vituo vya afya ili kuimarisha huduma bora kwa jamii, kwani serikali inatumia gharama kubwa katika kuangiza dawa, hivyo kamati za ulinzi na usalama vina wajibu wa kupata ripoti za uingizwaji na uotaji wa dawa ili kudhibiti changamoto hiyo.

"Tutafanya kila jitihada kuimarisha ukaguzi wa mara kwa mara katika hospitali zetu, haiwezekani wagonjwa wanakosa dawa kumbe kuna watumishi wachache wasio waaminifu wanaenda kuuza dawa zinazotolewa na serikali kwa watu binafsi," alisema. Awali akitoa taarifa ya CHF Mkoa wa Morogoro, Elisia Mtesingwa, alisema watu walioijunga na bima hiyo ni asilimia 9.4, huku lengo likiwa kufikia asilimia 30 hadi mwaka 2025.

Mtesigwa alisema changamoto kubwa wanayokutana nayo ni wananchi wengi kutokuwa na uelewa juu ya bima hizo na aina ya huduma inazotolewa, huku wengine wakilalamikia huduma mbaya wanazokutana nazo baada ya kutakata bima hizo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kusiyre Ukio, alisema wanatoa elimu kwa makundi mbalimbali wakiwamo wakuu wa wilaya, wakurugenzi na wataalamu wengine kufahamu namna ya kufuatilia mfumo wa uingizwaji wa dawa na kutoa dawa katika vituo vya kutolea huduma ili kuthibiti changamoto ya wizi wa dawa.



Mnufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) na mjasiriamali Elinita Mollel akiwa kwenye biashara yake ya kuuza nguo za mitumba, aliyoianzisha baada ya kupokea ruzuku ya TASAF, ilioko Ilkiding'a wilayani Arumeru. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Mradi wa teknolojia ya kilimo waleta mafanikio

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MRADI wa Maendeleo ya Teknolojia za Kilimo na Mifugo chini ya ufadhili wa Serikali za Tanzania na China umeleta mafanikio kwa wakulima wadogo wa mahindi na mpunga mkoani Morogoro.

Inaelezwa kufanikiwa kuongeza uzalishaji, hivyo kuongeza kipato na kuwa na uhakika wa chakula na kuuza ziada.

Mratibu wa Mradi huo, Ernest Mkongo, alisema hayo wakati wa ziara ya mafunzo mkoani Morogoro iliyofanywa na wanafunzi wa kitanzania wa masafa, kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha China.

Alisema mradi huo umeleta tija kwa wakulima wa vijiji vya Peapea, Mtego wa Simba, kwa kipindi cha miaka miwili ya awali tangu mwaka 2014,ambapo wakulima wa vijiji hivyo waliweza kupata mafanikio kwa kuongeza mavuno ya mazao hayo kutoka magunia manne ya mahindi kwa hekari moja hadi magunia 16.

"Baada ya mafanikio hayo ya mradi wa maendeleo ya teknolojia ya kilimo na mifugo kuwa wenye manufaa kwa wakulima wadogo eneo la mradi ulipanuliwa kutoka vijiji viwili vya awali na kuongeza vijiji vingine vinane," alisema Mkongo.

Mkongo alisema mradi katika Kijiji cha Mtego wa Simba, ulihusisha maendeleo ya vyuo vikuu, kikiwamo cha Kilimo cha China, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na serikali ili wakulima waweze kunufaika kwa kubadilisha maisha ya wananchi wa vijijini kupitia sekta ya kilimo yenye tija katika mfumo wa nguvukazi.

Ofisa Kilimo Mwandamizi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Evance Gambishi, alisema lengo kuu la mradi huo ilikuwa kukuza ukuaji wa uchumi kwa kuanzisha na kusambaza teknolojia za kilimo na mifugo kupitia uzoefu kutoka China ili kupunguza umaskini.

Alisema kuwa Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro,inatekeleza mradi huo kwa wakulima wadogo ili kupanua maeneo yao, hatua ambayo imesaidia kuongezeka kwa uzalishaji wa mahindi katika vijiji viwili vya majaribio baada ya wakulima kupewa mafunzo ya matumizi ya teknolojia ya China.

# Upanuzi wa HKMU wamkosha Makinda

**Na Joseph Mwendapole**

SPIKA mstaafu, Anne Makinda, amepongeza upanuzi unaofanywa na Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU) maeneo ya Boko jijini Dar es Salaam, kwani kutasaida kutoa wahudumu wengi wa sekta ya afya nchini.

Makinda ambaye kwa sasa ni Mkuu wa chuo hicho, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipokuwa akizungumza na wafanyakazi, walimu na wanafunzi wa chuo hicho ikiwa ni mara yake ya kwanza tangu ateuliwe kushika nafasi hiyo.

Alisema anakifahamu chuo hicho tangu kuanzishwa kwake, kwani kimekuwa kikifanya vizuri kwa kutoa wahitimu ambao wamekuwa wakifanya vizuri kwenye sekta ya afya katika maeneo mbalimbali nchini.

"Nampongeza Makamu Mkuu wa chuo kwa kutoa wahitimu bora na ambao wananidhamu sana kwa kweli huwa nakutana nao maeneo mengi wanayofanyakazi unaona kabisa huyu daktari au muuguzi amefundishwa na akafundishika. Endeleeeni kutoa huduma bora watu watawakimbilia," alisema

Aidha, Makinda ambaye alikuwa Spika wa Bunge 2010-2015 alipostaafu siasa, alisema amesikia changamoto ya mikopo kutoka kwa wanafunzi wa chuo hicho ambayo alisema ataifikisha kwa wahusika ili ifanyiwe kazi na waweze kuhudumiwa kama wengine.

"Mwenyekiti wa bodi aliwahi kuyasema haya mbele yangu kwamba wanafunzi hawa wakitoka hapa wanakwenda kufanyakazi kwenye hospitali za serikali sasa kwanini wakose mikopo, mimi nimelielewa na nitalifikisha kwa wahusika," alisema Makinda

Mwenyekiti wa Bodi ya Mtandao wa Elimu na Afya Kairuki (KHEN), Kokushubira Kairuki, aliiomba serikali isiwatoze pesa wanafunzi wa chuo hicho wanapokwenda kufanya mazoezi kwa vitendo kwani mwisho wa siku wanakwenda kulitumikia taifa la Tanzania.

"Tunapata shida wanafunzi wetu wanapokwenda kufanya mazoezi kwa vitendo kwani fedha wanazotaka ni kubwa nasisi hatuwezi kuwaongezea ada wanafunzi kufidia fedha hizo tunazotozwa hivyo tunaomba wasitutoze," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la chuo hicho, John Ulanga, alisema chuo kimeendelea kuongeza uwezo wa kufanya utafiti mbalimbali na kuongeza walimu wenye weledi wa hali ya juu hivyo kukifanya chuo kuendelea kuwa bora.

Alimpongeza Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof.Charles Mgone, kwa kuimarisha ubora wa ufundishaji hali inayokifanya chuo cha HKMU kuendelea kuwa miongoni mwa vyuo vikuu bora duniani na kwamba ndiyo sababu kinapata wanafunzi wengi kutoka nje ya nchi.

Nipashe
# TESA
Jumanne Julai 20, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

‘Inzi ni uhakika wa utajiri kwa vijana wabunifu’



Ukurasa 13

Inacholenga TPDC, vituo binafsi (2)



Ukurasa 14

**Wazazi, walezi watarajie haya wasipowaandaa mabinti kupevuka**

ELIMU

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# Ufunguo wa utajiri kwa kufuga samaki huu hapa

ELIMU ya ufugaji samaki inatajwa kuwa muhimu hasa kwa vijana ambao baada ya kuhitimu kila mwaka wanaendelea kukosa ajira.

Kujiajiri kwenye samaki kunawezekana kwenye maeneo tofauti yaliyo na vyanzo vya asili vya maji yakiwamo maziwa, mito hata bahari na pia kwenye mabwawa ya kuchimba ufugaji unawezekana hata kufanyika nyumbani.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Ugani na Uvuvi, Idara ya Utafiti Mafunzo katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Anthony Dadu, anasema ufugaji wa samaki unaoanza na elimu huwa na manufaa makubwa ikiwamo kipato.

Anasema ufugaji wa kisasa umeegemea kwenye teknolojia na kwamba upo utaalamu mwingi ambao mwananchi anayetaka kufuga akiihitaji hupata mafunzo bure huko Kingolwira, mkoani Morogoro.

Anasema ufugaji wa kwenye mabwawa kabla ya kuanza unahitaji uwepo wa maji ya kutosha katika eneo hilo.

“Tukishajiridhisha kwamba eneo lina maji ya kutosha tunatoa maelekezo ya nini cha kufanya mwanzo hadi fainali, atakamilisha bwawa na kuanza ufugaji,” anasema Dadu.

Anasema ufugaji huo unaangalia eneo lenye mita za mraba 600 urefu mita 30 na upana wa mita 20, ambalo kabla ya kuchimba linatakiwa kuwa wazi ili lituamishe maji.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Ugani na Uvuvi, anasema ili kubaini udongo unaotunza maji au mfinyanzi huchimbwa shimo dogo na kuwekwa maji na hufinyangwa kama mpira na kurushwa juu, iwapo utarudi chini bila kutawanyika, utakuwa bora kuanza ufugaji.

“Ufugaji huu wa mabwawa unahusisha samaki wa maji baridi kutoka mtoni, ziwani au ya kisima cha kuchimba. Angalizo kwa kisima cha kuchimba maji yake hayana oksijeni ya kutosha hivyo tunashauri akishayapandisha yawekwe kwenye bwawa lililoandaliwa kwa ajili ya kuyatunza lakini yasipelekwe kwenye samaki.”

Anashauri yakae kwa saa 24 ndipo yahamishiwe kwenye samaki baada ya kupata oksijeni ya kutosha na kwamba ufugaji huo ni wa kambare au sato.

### VIFARANGA

Maeneo mawili yaliyoko Dar es Salaam ya Big Fish Kigamboni na Eden Agriaqua iliyoko Chanika yanatajwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Ugani na Uvuvi, kuwa yana vibali vya wizara kuzalisha vifaranga vya sato na kambare.

“Wengine wapo Kibaha na Ruvu mkoani Pwani. Kumbukeni ili kifaranga kiwe tayari kufugwa ni lazima kiwe na gramu tano na kikilishwa chakula ipasavyo baada ya miezi sita ya kufugwa hufikia uzito wa nusu kilo tayari kuuzwa”.

### UWEPO WA SOKO

Dadu anasema soko ni kubwa Dar es Salaam na kwamba kuna wanunuzi wanaonunua kutoka kwa wafugaji na kuwachakata na kusambaza sokoni na kuongeza kuwa soko si shida, wafugaji ndiyo hakuna na kwamba bei ya sato ni Shilingi 6,000 kwa kilo.

### CHANGAMOTO

Dadu anasema tatizo lililopo katika ufugaji wa mabwawa ni kukosa elimu ya ufugaji, uhaba wa chakula na kwamba walio wengi huanza ufugaji huo kwa kuiga majirani au marafiki.



Mkufunzi kutoka Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Abdulmalik Kashaigiri (wa pili kulia), akitoa maelezo kwa wananchi jinsi ya kufuga samaki kwenye mabwawa, walipotembelea banda la wizara hiyo, katika maonyesho ya Sabasaba hivi karibuni. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

“Wengi wanaumia tatizo ni elimu hawana. Chuo cha mafunzo cha ufugaji samaki Kingolwira, kinatoa mafunzo ya kutosha bure kwa ambao ni kikundi wakijiunga tunawapa elimu,” anasema Dadu.

Anasema chakula kinachoshauriwa kwa samaki ni fish bean, soya bean, viazi, madini, dagaa ambavyo vikisagwa vinatoa chakula bora.

### ONGEZEKO LA SAMAKI

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, katika wiki ya chakula iliyofanyika Oktoba 10 hadi 16, mwaka jana, anasema sekta ya uvuvi inachangia asilimia 30 ya protini inayotokana na wanyama na inatoa ajira kwa Watanzania takribani milioni 4.5.

Anasema mwaka 2019/20, sekta hiyo ilikua kwa kiwango cha asilimia 1.5 na kuchangia asilimia 1.71 ya pato la taifa.

Pia uzalishaji wa samaki kutoka maji ya asili kwa mwaka 2019/20 umefikia tani 497,567 na katika uzalishaji wa mazao ya viumbe maji unafikia tani 18,717.

Kadhalika kumekuwa na ongezeko la uwingi wa samaki majini husuan katika Ziwa Victoria, sangara wameongezeka kutoka tani 417,936 mwaka 2016 hadi tani 816,964 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 95.5.

Dokta Tamatamah anaeleza kwamba uzalishaji na uvunaji wa samaki katika maji ya asili umeongezeka kutoka tani 362,645 mwaka 2015/2016 hadi tani 497,567 mwaka 2019/2020.

Anawataka wafugaji wa samaki kujifunza teknolojia mbalimbali za kisasa na kwamba ongezeko hilo la mazao ya uvuvi limetokana na dhamira ya serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wanaondokana na tatizo la uhaba wa chakula nchini husuan katika suala la upatikanaji wa protini ya samaki na nyama,” anaeleza Katibu Mkuu.

Aidha, Dk. Tamatamah anasema ongezeko hilo limetokana na chachu ya maadhimisho ambayo hukumbusha kila mwaka umuhimu wa kuwatendea haki Watanzania kwa kuhakikisha kuwa chakula cha kutosha kinapatikana, chenye ubora stahiki na kunalindwa ili kisiharibike kabla au baada ya kuvunwa na hatimaye kuliwa.

“Napenda kuwakumbusha wafugaji na wavuvi kuacha kuzalisha kwa mazoea. Tumieni teknolojia zilizopo kwenye mifugo, uvuvi na ukuzaji viumbe maji ili muweze kupata faida kwenye kazi zenu,” anasema Dk. Tamatamah.

SAYANSI/UBUNIFU

NA MWANDISHI WETU

# ‘Inzi ni uhakika wa utajiri kwa vijana wabunifu’

JUMATATU ijayo mataifa mbalimbali duniani yanakutana jijini Roma Italia kwenye makao makuu ya Shirika la Chakula Duniani (FAO), kujadili na kuamua namna mifumo bora ya chakula itakavyofanikisha kufikiwa malengo 17 ya maendeleo endelevu ya dunia, yanayotarajiwa kufikiwa mwaka 2030, ambayo msingi mkuu ni kila mmoja aweze kupata chakula cha kutosha na chenye lishe bora.

Baadhi ya malengo ya maendeleo endelevu (SDGs) yanayounganishwa na chakula moja kwa moja ni lengo la kwanza kupunguza umaskini, namba mbili kuondoa njaa, la tatu afya, nne la elimu, usawa wa kijinsia, jingine ni namba sita upatikanaji wa maji, namba nane ukuaji wa uchumi na SDG namba 2 matumizi na uzalishaji endelevu.

Ili kufikia malengo hayo ambayo ni makubaliano ya wanachama wa Umoja wa Mataifa, chakula ni suala lisilokwepeka kwa vile kuwapo umaskini ni matokeo ya watu kuishi na njaa, aidha afya duni huletwa na kukosa lishe bora, lakini bila kula na kushiba huwezi kuwa na elimu na upatikanaji wa maji (lengo namba sita) ni muhimu kwa vile ni rasilimali inayohitaji kutuzwa na kulindwa ili ifanikishe kilimo, ufugaji, uvuvi, uzalishaji viwandani na maisha bora ya jamii.

Ili kupata maoni ya wananchi kwenye kuandaa mifumo endelevu ya chakula shirika linalounganisha asasi za kirai zinazoshughulika na kilimo(ANSAF), liliandaa mjadala wa kitaifa wa chakula ulioishirikisha Wizara ya Kilimo, mashirika ya kimataifa kama Alliance for Green Revolution in Africa (AGRA) Vi-Agriforestry na kitaifa ya vijana kama NOV EED.

### MIFUMO YA CHAKULA

Mjadala wa taifa wa chakula unaitaja mifumo hiyo kuwa ni mnyororo mzima unaohusisha kulima mazao mashambani, ufugaji na uvuvi majini. Mingine ni uvunaji vyakula hivyo, usafirishaji, usindikaji viwandani, uhifadhi, utunzaji, uuzaji wake na kuandaliwa jikoni mwisho kuliwa mezani. Wajumbe wanakubaliana kuwa ili chakula kiwe na tija ni lazima kiwe na lishe bora na kiwe salama kutunza afya za walaji.

Akizungumza kwenye mjadala huo, Mkurugenzi Mtendaji wa ANSAF, Audax Rukonge, anasema serikali haiwezi kuzalisha ajira 1,000,000 kila mwaka kwa ajili ya wahitimu kutoka taasisi za elimu, hivyo suluhisho ni uwekezaji unaotumia ubunifu na teknolojia kwenye kilimo kuwezesha vijana kujiajiri.

Kwa mujibu wa taarifa za Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), kuna vyuo vikuu vya umma 12 , wakati vya binafsi ni 22, lakini vipo vingine vinavyosimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) na taasisi hizo huzalisha vijana kila mwaka ambao ni vigumu kupata ajira, kwa hiyo, uwekezaji kwenye ubunifu na kilimo unakuwa kipaumbele.

Ni katika mjadala wa kuandaa mifumo bora ya chakula, vijana mbalimbali wanaonyesha umahiri kuandaa mifumo endelevu ya kilimo inayolinda ikolojia na kimazingira ili kupata chakula bora na salama na pia kuinua kipato chao na cha jamii jirani, kama Diana Orembe kutoka Shirika la NOV FEED la Dar es Salaam, anavyoieleza Nipashe.

Akishiriki mkutano huo wa chakula, anasema shirika lao linaundwa na vijana wane wanaolima mboga, matunda na kufuga kuku pamoja na inzi ili kupata protini ya kutengeneza chakula cha samaki. Anasema wanawafuga inzi chuma (black solders) wanaotaga mayai ambayo huzalisha funza ambao ni chakula cha samaki na kuku.



Diana Orembe, akikagua protini au funza wanaotumiwa kutengeneza chakula cha kuku na samaki badala ya dagaa na maharage ya soya ambayo ni chakula cha binadamu. **PICHA: NOVFEED.**

> “Ubunifu wetu unatumia teknolojia rahisi mfano tunatumia mabaki ya vyakula, matunda na mboga yanayoliwa na inzi ambao hutaga mayai. Funza nao hula mabaki hayo na kati ya siku 10 hadi 14 tunakuwa tumepata protini hiyo. Tunaikausha na kuuzia wafugaji.” Anaongeza.

“Tunazalisha tani moja ya funza kwa mwezi na tunawauzia wafugaji wa samaki na kuku. Kilo moja ni Sh 2,300. Tulianza tangu 2017 kufanya utafiti na tumeanza kuzalisha mwaka huu,” anasema Diana mhitimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akisoma shahada ya sayansi kuhusu viumbe wadogo (microbiology) na kwamba alifundishwa ujasiriamali UDSM na sasa anashirikiana na wajasiriamali wenzake waliohitimu Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo(SUA).

### KWANINI KUFUGA INZI?

Diana anasema samaki na kuku wanalishwa chakula cha binadamu soya na dagaa, hivyo pengine si jambo jema, lakini funza hao wanakuwa mbadala wa vyakula vya binadamu na lengo lao ni kuwapa wafugaji chakula bora cha mifugo kwa bei nafuu.

“Ubunifu wetu unatumia teknolojia rahisi mfano tunatumia mabaki ya vyakula, matunda na mboga yanayoliwa na inzi ambao hutaga mayai. Funza nao hula mabaki hayo na kati ya siku 10 hadi 14 tunakuwa tumepata protini hiyo. Tunaikausha na kuuzia wafugaji.” Anaongeza.

Anafafanua kuwa mabaki ya chakula kilicholiwa na funza ni mbolea ya bustani za mboga za NOVE FEED zenye matunda, nyanya, mchicha, spinachi, ngogwe, pilipili hoho nyekundu, za kijani na njano.

Anasema wanatumia mbolea za mboji na samadi na viuatilifu vyao ni vya asili kutoka kwenye mimea na wanavvyovitengeneza wenyewe ili kulinda mifumo ya chakula, maji, ardhi na pia kuzalisha chakula kwa njі zisizohusisha matumizi ya kemikali na sumu (organic) .

### KUSHIRIKISHA JAMII

Diana anasema pamoja na kuwauzia wafugaji chakula cha mifugo pia wanawapa kinamama mchicha, spinanchi na ngogwe zinazozalishwa bila kemikali ili kuziuza lakini wanatakiwa kuweka fedha kwanza, kusajiliwa na kuwa sehemu ya mtandao wa wafanyabiashara kabla ya kuzifikisha sokoni.

“Ubunifu wetu umeajiri vijana watatu, wanaozalisha inzi, wengine saba wanaokusanya mabaki ya vyakula, matunda, mboga na bidhaa nyingine zinazofaa kuwalisha inzi pamoja na protini au funza,” anasema.

Anasema kazi hizo zinafanikishwa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Ubungo, taasisi ya CHEMONIC ya Marekani na benki za biashara.

Oktoba mwaka jana Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilieleza kuwa sekta ya uvuvi inachangia asilimia 30 ya protini inayotokana na wanyama na inatoa ajira kwa Watanzania takribani milioni 4.5, hivyo inahitaji uwekezaji zaidi.

TEKNOLOJIA

**NA MWANDISHI WETU**

# Inacholenga TPDC, vituo binafsi (2)

## • Ndivyo mbadala dizeli, petroli unavyofanya kazi

LEO tunakamilisha makala ya magari yanayotumia gesi badala ya dizeli na petroli ukiwa ni mkakati wa kidunia wa kupunguza joto na taka sumu zinazozalishwa na injini za magari.

Mataifa yaliyoendelea kiuchumi injini za magari zimebadilishwa kutumia umeme na gasi ili kupunguza uchafuzi wa mazingira unaochangia ongezeko la joto duniani. Tanzania haijabaki nyuma, juhudi zinaendelea zikifanywa na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) na kampuni binafsi ya PanAfrica Energy (PAET), kama anavyoeleza Mkurugenzi wa Biashara ya Mafuta na Gesi wa TPDC, Dk. Wellington Hudson, katika mahojiano na Nipashe.

Anaanza kueleza maana ya gesi CNG kuwa ndiyo inayotumiwa kwenye injini za magari na kwamba 'CNG' ni kifupisho cha 'Compressed Natural Gas' ambayo ni gesi asilia iliyoshindiliwa katika mgandamizo mkubwa ili kuhifadhi kiasi kikubwa cha nishati hiyo kwenye mtungi na ndiyo inayotumika na injini. Endelea na mahojiano.

**SWALI:** Ni magari mangapi leo yameshabadilishiwa injini ili kutumia CNG?

**JIBU:** Yapo zaidi ya 700, ambayo yameshawekewa mfumo wa CNG na yanatumima gesi asilia. Mengi ni ya watu binafsi na idadi kubwa ni yaliyo katika mtandao wa kutoa huduma za usafiri ya kampuni za UBER na BOLT.

**SWALI:** Hadi sasa ni mikoa mingapi ina vituo vya CNG?

**JIBU:** Ni Dar es Salaam na Mtwara pekee, Dar es Salaam kituo kinapatikana Ubungo Maziwa wakati Mtwara kipo ndani ya kiwanda cha saruji cha Dangote, kampuni ilikijenga kuhudumia magari ya kusafirisha saruji.

**SWALI:** Nishati ya CNG inaweza kuharibu injini?

**JIBU:** Hapana haiharibu injini badala yake husaidia kuongeza uhai au muda wa matumizi ya injini kwa sababu huiongezea ufanisi mkubwa na hutumia nishati kidogo. Aidha, huzalisha kiasi kidogo cha hewa ukaa na kwenye injini haibakizi mabaki ya kaboni.

**SWALI:** Ni magari gani yanayoweza kubadilishwa au kuwekewa mfumo wa CNG?

**JIBU:** Karibu magari yote yanayotumia petroli yanaweza kubadilishwa au kuwekewa mfumo wa kutumia gesi asilia. Kawaida mfumo wa petroli katika magari hubakia kama ulivyo, ila huongezewa mfumo wa kutumia CNG. Mtumiaji anaweza kutumia petroli anapoishiwa gesi au kuchagua kutumia kimojawapo mafuta au gesi, kwa kubonyeza kitufe kinachowekwa kwenye 'dash board' ya gari.




Ndivyo mitungi ya gesi asilia inavyohifadhiwa ndani ya buti la gari linalotumia gesi. **PICHA MTANDAO**

**SWALI:** Unahitajika muda gani kubadilisha au kuweka mfumo wa CNG kwenye gari?

**JIBU**: Kwa wastani inaweza kuchukua siku moja hadi mbili. Lakini, muda wa kuweka mfumo wa CNG kwenye gari hutegemea na aina ya mfumo wa gari pia na idadi ya wafanyakazi kwenye karakana.

**SWALI:** Mitungi ya CNG inawekwa wapi? Inaweza kupunguza nafasi kwenye gari ?

**JIBU:** Inawekwa kwenye buti. Gari dogo linaweza kuwekewa mtungi mmoja wa kilo 15 au miwili ya kilo 7.5 kila mmoja. Hivyo, kiasi cha ujazo (ukubwa) wa buti hupungua kwa sababu ya nafasi inayochukuliwa na mitungi.

**SWALI:** Gari la injini ya CNG lina masharti yoyote ya kuegesha?

**JIBU:** Linaweza kuegeshwa sehemu yoyote ambayo inaruhusiwa kuegesha magari. Hakuna vikwazo vyovyote vilivyowekwa kwa ajili ya kuegesha gari lenye mfumo wa CNG, kwenye maeneo ya maegesho yaliyoruhusiwa kisheria.

**SWALI:** Inagharimu Shilingi ngapi kuweka mfumo wa CNG kwenye gari la petroli na taasisi ipi inahusika?

**JIBU:** Gharama hutegemea mambo mengi ikiwa ni pamoja na aina ya gari na uingizaji wa mafuta kwenye injini, aina ya vifaa vya mfumo wa CNG vitakavyofungwa, idadi ya mitungi ya gesi na ukubwa wake.

Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) ndiyo pekee yenye karakana ya kuweka mfumo wa CNG kwenye gari na gharama hutegemeana na idadi ya silinda za injini. Silinda 3 ni Shilingi milioni 1.5, nne ni milioni 1.85 wakati silinda 6 hugharimu milioni 2.35 na zikiwa nane gharama yake ni Sh milioni 2.7. Kwenye gharama hizi mteja anaongeza asilimia 18 ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

**SWALI:** Usalama wa gari la mfumo wa CNG ukoje?

**JIBU:** Mfumo unaofungwa hukaguliwa na mtaalamu wa mifumo ya gesi kwenye magari kabla halijaanza kuwekewa au kutumia gesi baada ya kuwekewa mfumo wa CNG. Lengo ni kuhakikisha kuwa umefungwa ipasavyo na ni salama kwa matumizi.

Mitungi ya gesi imewekewa muda wa mwisho wa matumizi (expiry date), hivyo muda huo unapofika hairuhusiwi kutumika tena. CNG inaongezewa kemikali ya kuiwezesha gesi kuwa na harufu ili pindi inapokuwa inavuja, iwe rahisi kugundua uvujaji wa gesi hiyo kabla haijasababishia madhara.

**SWALI:** TPDC itaanza lini kusambaza CNG mikoa mingine mbali na Mtwara na Dar es Salaam?

**JIBU:** Mpango wa kufikisha gesi asilia mikoani umeshaanza, TPDC inakusudia kujenga miundombinu ya vituo vya kushindilia gesi katika mitungi maalumu na kuisafirisha kwa magari, treni na meli hadi mikoani.

Mshauri mwelekezi amekamilisha michoro ya usanifu wa mradi na shirika linatumia zabuni kupata makandarasi wa ujenzi wa vituo hivyo.

Aidha, TPDC inakusudia kuanza kusambaza gesi mikoani kwa kutumia njia ya kuishindilia kwenye mitungi maalumu ama kuibadilisha gesi na kuwa ya kimiminika na kuisafirisha kwa magari, treni au meli hadi mikoa hiyo.

Teknolojia hii inalenga kuifikisha gesi mikoani katika muda mfupi ujao hadi ujenzi wa miundombinu ya mabomba ya kuisafirishia itakapokamilika.

**SWALI:** Kuna mkakati gani kuongeza vituo vya kujaza CNG kwenye magari, mbali na kimoja kilichopo Ubungo Dar es Salaam?

**JIBU**: Mpango wa kuongeza vituo vingi zaidi kurahisisha upatikanaji wa huduma hii kwa wateja wengi umeshaanza ambapo kwa kuanzia vituo viwili mama na vidogo vitatu vya kupokelea gesi vimeanza kujengwa na vitawekewa mfumo wa kujaza gesi kwenye magari.

Aidha, serikali inashirikisha kampuni binafsi zenye vituo vya mafuta, ili zifunge pampu za kujaza gesi kwenye magari katika vituo vyao na kampuni 10 zimeonyesha nia ya kufanya biashara hiyo na zimeshapata vibali vya kufanya biashara hiyo, na hatua inayofuata ni kampuni hizo kuomba vibali kutoka EWURA ili kujenga vituo au kuweka pampu hizo na kisha kupata leseni ya kuendesha biashara hiyo.

**SWALI:** Wataalamu wa kubadilisha injini hizo wapo wa kutosha? Na wanafundishwa na vyuo gani?

**JIBU:** Hadi Juni 2021 kampuni 10 zilikuwa zimepata idhini ya TPDC kushiriki biashara ya gesi kwenye magari ikiwa ni pamoja na kujenga vituo vya kuyajaza gesi asilia. Kati ya kampuni hizo sita zimepata idhini ya kujenga karakana za kuongezea mfumo wa gesi kwenye magari yanayotumia ama petroli au dizeli.

Aidha, kampuni hizo zinadhibitiwa na Bodi ya Makandarasi (CRB) na zinapaswa kutoa mafunzo zenyewe ili kujiridhisha na utendaji kazi wao. TPDC linatoa wito kwa kampuni nyingine kutumia fursa hii ili kuingia kwenye biashara hii.

AFYA

NA GEORGE MAPUNJO

# Wazazi, walezi watarajie haya wasipowaandaa mabinti kupevuka

LINAPOTAJWA suala la afya, hakuna mbadala, linamhusu kila mmoja bila kujali, utajiri, umaskini, utaifa wala umri. Na kwa kinamama na watoto ni jambo nyeti zaidi kwa vile linahusisha ujauzito, uzazi na makuzi ya watoto.

Afya ndiyo msingi wa utekelezaji wa malengo 17 ya maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa (UN -SGDs) na linaibuka kuanzia lengo la kwanza la dunia isiyo na umaskini, la tatu afya, la nne elimu, namba tano ni usawa wa kijinsia, wakati la sita linahusu upatikanaji wa maji, lengo la nane linagusa ukuaji wa kiuchumi unaohusisha uendelevu wa ajira zenye staha, lengo namba 11 ni kuwa na makazi endelevu wakati lile la 12 ni matumizi na uzalishaji endelevu.

Muhimili mkuu wa SDGs ni afya na kwa wanawake na mabinti suala la hedhi salama lina nafasi yake kwenye malengo hayo, hivyo badala ya kulifanya kuwa siri na mwiko ndani ya jamii ni wakati wa kuanza utaratibu wa kuwaandaa na kuwaelimisha mabinti kuhusu hedhi salama wanapokaribia kupevuka.

Hedhi isiyo salama inaathiri afya husababisha maradhi ya kuambukizwa na kwamba magonjwa ya uzazi hayaonekana mapema, mpaka unapofikia wakati wa kupata mtoto na wakati mwingine kisababishi ni kutumia njia zisizo sahihi wakati wa hedhi.



Mabinti waelimishwe habari za hedhi salama wanapokaribia kupevuka kuepusha hamaki na magonjwa. **PICHA: MTANDAO**

Dk. Daniel Mpembeni, anasema baadhi ya magonjwa hayo ni kuziba mirija ya uzazi, mfuko wa uzazi kushindwa kubeba mimba, maumivu wakati wa kupata haja ndogo, kusinyaa kwa viungo vya uzazi, maumivu wakati wa kujamiiana, kujihisi kutokuwa sawa muda wote, kupata maambukizi ya njia ya mkojo (UTI) hata saratani.

Mpembeni, anawashauri wazazi, walezi, walimu na jamii kuwapa mabinti elimu ya hedhi salama wanapoona umri wa kupevuka unakaribia ili kuepukana na matatizo mbalimbali ya kiafya na hata kuwasababishia ugumba.

Mabinti ambao hawajapata elimu ya hedhi salama na jinsia wanapata taabu zaidi wanapofikia umri wa balehe, kama wanavyosema baadhi ya wanafunzi wa sekondari waliokuwa wanashiriki kwenye maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama, Mei mwaka huu.

Wanaamini wazazi na walezi wanajibika kuwafahamisha watoto wa kike na kiume elimu ya jinsia kama njia mojawapo ya kuwanusuru dhidi ya magonjwa na mabadiliko ya kimwili.

"Matatizo mengi ya vijana na wasichana huanza wanapoanza kubalehe hapa ndipo tunahitaji kuhakikisha kwamba wasichana na wanawake wanafikiwa na miundombinu rafiki ya hedhi kwa afya na usafi." Anasema Dk. Mpembeni.

Mwanafunzi wa kidato cha tatu, Clara Minja, anasema anajisikia vibaya ikifika siku za hedhi na kutamani iwepo njia mbadala ili asizifikie kutokana na maumivu makali hata kushindwa kwenda shuleni.

Neema Godfrey, anasikitika kuwa alipata hedhi ya kwanza bila kufahamu chochote kuhusu hali hiyo hadi mama alipomwambia: "Mwanangu umekuwa sasa" hivyo unahitaji kuwa safi wakati wote kimwili na kiakili na ujiepushe na mienendo mibaya ya ngono".

Na Getrude Tingisha anasema: "Wazazi, walezi na walimu wanatakiwa kutoa elimu kuhusu jambo hili, ni tatizo na wengi wetu hatujui kuhusu hedhi salama na cha kufanya inapotokea katika mazingira yoyote."

**WAZAZI WANAVYOJITETEA**

Kwa upande wa wazazi wanaozungumzia hedhi salama wanasema gharama kubwa za maisha zinawakwamisha kumudu kununua taulo za kike kwa mabinti, hivyo kutegemea zaidi njia mbadala kama vitambaa ambayo wengi wanasema si salama.

"Pamoja na changamoto kuna jukumu la kuwalea watoto kimaadilii na kuwaeleza hali halisi wanapofika umri wa kuvunja ungo ili kuwaepusha na matokeo mengine kama kupata mimba utotoni ," anasema Fortunatha John, mkazi wa Salasala Dar es Salaam. Pili Kande mzazi wa mabinti kadhaa na mkazi wa Mwandege na mfanyabiashara wa Kariakoo anayeuza taulo za kike, anasema ingawa kodi zilionolewa na sasa zimerudishwa, wanalazimika kuziuza kwa bei juu kufidia gharama kwa vile hata wazalishaji wanawauzia ghali.

"Mimi ni mama na nina watoto wa kike, inanilazimu kuuza kwa gharama ili kupata faida. Vilevile, wateja wanapokuja kununua bidhaa hizi, tunawapa elimu kuhusu matumizi sahihi ya taulo pamoja na usafi binafsi." Anasema Pili.

Maadhimisho ya hedhi salama hufanyika kila mwaka Mei 28, tangu yalipoanzishwa rasmi mwaka 2014 na Umoja wa Mataifa (UN), na kwamba ni siku muhimu ya kujenga uelewa na kupaza sauti kuhusu upatikanaji wa huduma bora na saidizi kwa wanawake wanapokuwa kwenye siku zao.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni "utendaji na uwekezaji katika hedhi safi na afya kwa ujumla' jambo linalohusisha pia kuvunja ukimya, kushawishi watunga sera, waandaa bajeti za kutosha kuwezesha upatikanaji wa taulo za kike na vifaa vingine, vyoo vya kutosha na majisafi na salama kupatikana kwa wote.

Shirika la TGNP Mtandao ni wadau wa hedhi salama na walikuwa kampeni ya "Wape Mabawa" ambayo ilileta matokeo chanya, kwani baadhi ya halmashauri kama Mbeya, Kishapu, Kisarawe, Morogoro na Ilala walikuwa na bajeti zilizoonyesha kuwa wana nia ya dhati ya kukabiliana na changamoto hizo.

Halmashauri hizi zinatenga fedha za makusanyo ya ndani kuboresha miundombinu ya vyoo ili kukidhi mahitaji ya wasichana wanapokuwa kwenye hedhi na kutoa pedi bure shuleni.

Kwa mujibu wa Wizara ya Elimu ni asilimia 11 tu ya shule ndiyo zina vyoo bora, aidha utafiti wa Shirika la SNV la Uholanzi wa mwaka 2014 ulibaini kuwa asilimia 99 ya shule hazina huduma ya maji wala vyumba vya kubadilishia wakati wa hedhi. Wakati utafiti wa Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) wa 2009 ulionyesha kwamba asilimia 4 ya shule ndiyo zina vyoo kwa ajili ya watoto walemavu. Ili kujenga heshima kwa hedhi salama, wadau wa jinsia ya maendeleo wanatakiwa kuishawishi serikali na halmashauri kuhakikisha shule zina vifaa maalumu vya kuhifadhi au kuteketeza pedi zilizotumika ndani ya vyumba maalumu shuleni.

Utafiti wa Taasisi ya Taifa ya Tiba (NIMR), unaonyesha kwamba asilimia 63 ya vyoo vya shule hazina vyombo vya kuhifadhia pedi zilizotumika. Asilimia 38 za shule hazina maji wakati asilimia 46 hazina mfumo wa maji unaofanya kazi, asilimia 57 ya shule hazina maji ya kutosha na asilimia 99 za shule hazina sabuni kwa ajili ya kunawia mikono, asilimia 98 za shule zina idadi ndogo ya sehemu ya kunawia mikono, faragha na mahali pa kuhifadhia taka (NIMR, 2016).

Mkurugenzi wa Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA), Rose Reuben, anasema suala la hedhi salama siyo la mwanamke peke yake bali ni la jamii yote kwani likiwa ni suala la mwanamke pekee jamii haitakuwa na usawa wa kijinsia kama lengo la tano la malengo endelevu ya dunia. "Hali ya hedhi ni ya kibaiolojia lakina inaweza kumkwamisha mwanamke kushindwa kufikia ndoto zake iwapo inapotokea kumkwamisha mtoto kwenda shule.

Suala la hedhi salama lifahamike kama wengine wanavyoijua mipira ya kondomu ambayo ipo kila sehemu kwa sababu inapunguza maambukizi ya magonjwa mbalimbali na kuzuia mimba. Ifike mahali taulo za kike nazo ziwekwe kila sehemu iwe katika vyoo vya watu binafsi au umma ili iwe rahisi watu wengi kuzipata.



# Jiji lapewa jukumu uhaba wa madarasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imeagizwa kushughulikia tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa na vyoo vya walimu katika Shule ya Msingi Michese.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alitoa agizo hilo jana, baada ya kubaini kuna mrundikano wa wanafunzi kwenye madarasa, huku walimu wakilazimika kuchangia vyoo na wanafunzi.

Mtaka alisema ni aibu shule hiyo kuwa katikati ya Jiji na haina hadhi na kulitaka Jiji hilo kukarabati miundombinu ya shule hiyo ikiwamo madarasa, nyumba za walimu, vyoo na huduma ya maji.

"Katika karne hii kweli bado kuna shule ambazo wanafunzi wanakaa chini? Lazima sisi kama viongozi tuzitendee haki nafasi zetu katika kutoa huduma hasa katika masuala ya elimu ili watoto wetu wasome kwa ari," alisema.

Alisema ili kuwa na ufaulu mzuri lazima miundombinu ya elimu iwe mizuri.

"Nakuomba Mkurugenzi wa Jiji ushughulikia changamoto hiyo ya uhaba wa vyumba vya madarasa kwani tayari serikali ilishapitisha bajeti ya elimu hivyo katika fedha watakazopokea wahakikishe wanaifikia shule hii."

"Ili kuwe na ufaulu mzuri lazima miundombinu ya elimu iwe mizuri hasa ukizingatia kumekuwa na ugonjwa wa Covid-19 na wanafunzi wengine kukaa chini kwa ukosefu wa madawati hii kwetu ni aibu," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wazazi kuacha kuwapa watoto majukumu mengi ya kazi za nyumbani na badala yake waachie muda wa kujisomea.

"Hapa kuna baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa wakiwatumikisha watoto kufanya kazi za nyumbani kama kuosha vyombo, kufua, kuchota maji na kuwafanya watoto kuchoka, wanashindwa kupata muda wa kujisomea hasa wenye watoto wa madarasa ya mitihani ya darasa la nne na la saba," alisema.

Awali, akitoa taarifa kwa Mtaka, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Sizya Wiliam, alisema shule ina wanafunzi 1,850, vyumba vya madarasa tisa na upungufu wa madawati 100.

Alisema kuna uhaba wa vyoo vya walimu ambapo kwa sasa wanajisaidia kwenye vyoo vya wanafunzi au kwa majirani wa shule hiyo.

"Ni jambo la aibu kwetu, shule yetu inakabiliwa na changamoto nyingi kama unavyoona, mrundikano katika vyumba vya madarasa na pia tuna uhaba wa madawati hata hivi vyumba vya madarasa tisa vilivyopo ni chakavu kabisa," alisema.

Pia alisema idadi ya walimu waliopo haiendani na wanafunzi hali inayochangia kushuka kwa ufaulu shuleni hapo.



Wachuuzi wa Kimasai wakiuza tangawizi eneo la Oneway jijini Dodoma jana, huku wakihudumia wateja wao. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Waonya kuwaepuka matapeli wa ardhi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKAZI wa Jiji la Dodoma wametahadharishwa kujiepusha na madalali ambao wamekuwa wakiwashawishi kuuza ardhi yao kwa bei ndogo.

Naibu Meya wa Jiji hilo, Emmanuel Chibago, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wakazi wa Mtaa wa Chilwana, Kata ya Ihumwa kwenye uzinduzi wa kazi ya ufunguaji na uchongaji wa barabara unaofanyika na kampuni ya Makazi Solutions (T) LTD.

Chibago alisema badala ya kuyauza maeneo yao, waitumie ardhi hiyo kwa kuiboresha ili kuondokana na adha za kushawishiwa na vishoka na kuuza kwa bei ndogo.

Alisema ni vyema wakatumia ardhi yao kubadilisha maisha badala ya kudanganyika na vishoka ambao kila siku wamekuwa wakizunguka kwenye maeneo mbalimbali yanayopimwa na kwenye mashamba.

"Ninawaomba nyinyi ndugu zao wa huu Mtaa wa Chilwana, ambao leo hii mmepimiwa ardhi yenu pamoja na kuchongewa barabara, kamwe msidanganyike kuyauza maeneo yenu badala yake boresheni kwa kujenga nyumba za kisasa kuliko kukubali pesa ndogo inayotolewa na hawa vishoka ambao kutwa mzima wanazunguka mitaani na mashambani," alisema.

Aliwataka watendaji wa kampuni hiyo kuhakikisha migogoro na migongano kwenye utendaji wao wa upimaji wa ardhi kutatua ili wapate ushirikiano kwa wakazi hao. Alisema kwenye utendaji wao wa upimaji na uchongaji wa barabara kuna wakazi wanaopitiwa na miundombinu mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya eneo husika, hivyo hakuna sababu ya kuwapo kwa migogoro isiyo kuwa na tija badala yake toeni elimu itakayotambua umuhimu wa kuwapo kwa miundombinu hiyo.

Naye Meneja wa mradi huo, Pazi Said, alisema wamepanga viwanja 6191 vyenye matumizi mbalimbali vikiwamo maeneo ya makazi 4500, makazi na biashara 1355, biashara 121, huduma za kijamii 88, viwanda vidogo vidogo, shule, zahanati, vituo vya afya, nyumba za kuabudu na ya uwazi.

Said alisema mpaka sasa kampuni hiyo imefanikiwa kupima viwanja 5,300 sawa na asilimia 85.6 ya viwanja vyote vilivyopimwa.

## Serikali yatakiwa uwekezaji kwa wahitimu kilimo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kuwekeza kwa vijana waliohitimu vyuo vya kilimo, kikiwamo Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), ili wawe na mashamba ya mfano yatakayosaidia kuwashawishi jamii kuwekeza.

Mtaalamu wa kilimo na mifugo, Abdul Kafuku, alitoa ushauri huo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uwekezaji wa masuala ya kilimo nchini.

Kafuku alisema serikali na wanasiasa wanatakiwa kuendelea kuhamasisha vijana kushiriki kilimo hususani wale waliobobea katika taaluma hiyo na itatoa hamasa kwa jamii kufanya kilimo hasa cha kibiashara ili kujiinua kiuchumi.

"Serikali ingefikiria namna ya kuwapatia maeneo ya kilimo na mitaji kwa ajili ya kuendesha kilimo cha mfano ili vijana wengine wajifunze kutoka kwao," alisema.

Aliongeza: "Kilimo kinalipa lakini unatakiwa ujue unalima nini na soko lipo wapi ndio maana nasisitiza wawekeze kwa vijana wenye taaluma ya kilimo ili wasaidie kutoa darasa kwa wengine."

Alisema Tanzania ina ziada ya chakula baada ya kuzalisha asilimia 136, lakini kama vijana wakishirikishwa kikamilifu na wakapenda kilimo kutakuwa na chakula cha kutosha na hata kuuza mazao mengi zaidi nje ya nchi.

Kwa upande wake, Mtaalamu wa Kilimo ambaye ni Ofisa Kilimo mstaafu, Aithan Chaula, alisema vijana wanatakiwa kuaminishwa kuwa kilimo kinalipa.

Alisema vijana wanataka kuona mfumo wa kilimo unaoeleweka ili wafanye kilimo kazi kama kazi nyingine.

Chaula ambaye ni Katibu Mtendaji wa Shirika la Agriculture Seeds Production Association (DASPA), alisema "Wakati mwingine serikali ifike mahali iingize mkono wake kuwasaidia vijana wanaowekeza kwenye kilimo."

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Sagara, Wilaya ya Kongwa, Gilbert Mlwande, aliitaka serikali kuongeza juhudi katika kuwasaidia wakulima hasa upande wa upatikanaji masoko ya uhakika.

Alisema kama wakulima waliopo vijijini watasaidia upande wa masoko itasaidia kwa kiasi kikubwa kuhamasisha vijana kuingia kwenye kilimo.

Alisema vijana wengi hawapendi kushiriki kilimo kutokana na kukosa mitaji hali inayofanya wajikite katika shughuli nyingine.

Mkulima katika kitongoji cha Ng'humbi, Baraka Maire, alisema serikali iwezeshe kilimo cha umwagiliaji ili kuwe na ufanisi mkubwa.

"Tuangalie namna ya kuchota maarifa yaliyopo kwa wabobezi na wataalamu wa kilimo badala ya kufikiria tuma maofisa ugani walioajiriwa na serikali," alisema Maire.





# Wito wakulima mpunga kuchangia gharama

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKULIMA wa mpunga katika Skimu ya Mwendamtitu wilayani Mbarali, wametakiwa kuchangia gharama za uendeshaji na uboreshaji wa miundombinu ya skimu hiyo, ili iwasaidie kuondokana na uhaba wa maji unaosababisha mazao kukauka.

Aidha, wakulima hao wameshauriwa kutotegemea mvua kwenye uzalishaji wa mpunga kutokana na mabadiliko ya tabianchi, ambayo yamesababisha wakati mwingine mvua kutokuwa ya uhakika na hivyo kusababisha mazao kukauka.

Ushauri huo ulitolewa na Ofisa Kilimo anayeshughulikia mazao wilayani Mbarali, Jamson Mwailana, kwenye maadhimisho ya Siku ya Mkulima wa Mpunga wilayani humo yaliyofanyika katika Kijiji cha Mwendamtitu.

Alisema katika skimu hiyo kila mwaka unatokea ukame, ambao unaathiri mazao yao kutokana na mchanga kuziba mfereji na kusababisha maji yasifike kwenye mashamba ya wakulima, na kwamba wakati mwingine usafishaji wa mfereji unacheleuwa kutokana na wakulima kutochangia gharama.

"Nawaomba ninyi ambao mmefika kwenye maadhimisho haya mkasaidie kuhamasisha wenzenu huko, fedha zitolewe kwa wakati ili kazi ya kuiendesha skimu yetu iwe nyepesi na tuhudumie mazao yetu kwa wakati," alisema Mwailana.

Alisema wakulima hao ndio wanufaika wa skimu hiyo, hivyo wanatakiwa kushiriki kuihudumia ili iwasaidie kuongeza uzalishaji na kuinua uchumi wao pamoja na kuwa na uhakika wa chakula. Mratibu wa skimu hiyo, Bruno Mgumba, alisema gharama wanazopaswa kuchangia wakulima hao ni Sh. 50,000 kwa kila ekari moja na kwamba gharama hizo zimepangwa na serikali.

Alisema serikali ilipanga gharama hizo kwa kuzingatia bei ya chini ya mpunga kwa maelezo kuwa gharama hizo ni sawa na bei ya gunia moja la zao hilo.

Alisema uendeshaji wa skimu za umwagiliaji ni kubwa katika baadhi ya maeneo, lakini kwa Wilaya ya Mbarali skimu nyingi gharama zake ni za kawaida, kutokana na jiografia yake kuwa ya tambarale maeneo mengi.

"Asilimia 70 ya gharama hizo hutumika katika kukarabati miundombinu ya skimu hii na asilimia 30 hutumika kwenye uendeshaji, tatizo ambalo huwa linatokea ni baadhi ya wakulima kutochangia kwa wakati na wengine kutochangia kabisa," alisema Mgumba.

Baadhi ya wakulima wanaotumia skimu hiyo walisema wakulima wenyeji huwa wanachangia bila tatizo, lakini tatizo huanzia kwa wakulima wageni, ambao huwa wanakodi mashamba ama kuyanunua kutoka kwa wenyeji. George Morice, alisema wengi wao siyo waelewa, hivyo kushindwa kukubali kuchangia gharama za uendeshaji wa skimu. Aliwaomba viongozi wa serikali watoe elimu zaidi kwa wakulima hasa msimu wa kulima, ambapo kila mkulima hupatikana shambani.

Alisema kutokana na mfereji wa skimu hiyo ulivyo pamoja na miundombinu yake, bado gharama ya Sh. 50,000 ni ndogo kwa maelezo kuwa fedha hizo hazitoshi kuendesha skimu.



Mbunge wa Momba mkoani Songwe, Condester Sichalwe, akisikiliza mahitaji ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Ikana ambao walimwomba mbunge huyo msaada wa mahitaji mbalimbali kama vile viatu, madaftari na mabegi ya shule jana, wakati watoto hao wakielekea shuleni. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Mbunge Chunya: Wananchi shirikini kwenye ujenzi miradi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MBUNGE wa Lupa katika Wilaya ya Chunya, Masache Kasaka, amewataka wakazi wa wilaya hiyo kushiriki kwenye ujenzi wa miundombinu ya elimu na afya kwenye maeneo yao ili kuishawishi serikali kupeleka fedha za miradi.

Alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara katika Kata ya Matwiga na kuzungumza na wananchi hao, ambapo alichangia mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Matwiga na mifuko mingine 50 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mwalimu katika Shule ya Msingi Mazimbo.

Alisema serikali kwa sasa ina utaratibu wa kujenga miundombinu kwa kushirikiana na wananchi, akisema kuwa miradi mingi inaibuliwa na wananchi na kadri inavyoendelea serikali inashawishika kupeleka fedha za kukamilishia.

Alisema wananchi wanatakiwa kujenga maboma ya shule na zahanati kisha serikali inayakamilisha kwa kuyaezeka na kukamilisha maeneo yote ambayo yanakuwa yamebakia.

"Sisi ndio wenye shida huku kwetu na sisi ndio tunayajua matatizo yetu kwamba tunatembea umbali mrefu kwenda kupata matibabu, kwa hiyo sisi ndio tunatakiwa tuwe mstari wa mbele kujenga miundombinu hii, tukishamaliza boma tunaandika barua kwa mkurugenzi anakuja kumalizia," alisema Kasaka.

Alisema endapo wananchi wataendelea kusubiri serikali ifanye kila kitu, watakuwa wanajicheleweshea maendeleo wenyewe na wataendelea kupata shida, huku wakishuhudia maendeleo kwenye maeneo mengine.

# Walalamikia lumbesa biashara ya viazi mviringo

**Na Nebart Msokwa,** MAKETE

WAKULIMA wa viazi mviringo wilayani Makete katika Mkoa wa Njombe, wamelalamikia wafanyabiashara kuendelea kuwalazimisha kununua mazao yao katika magunia ya ujazo mkubwa maarufu kama lumbesa kwa bei ndogo.

Wakulima hao wamekiita kitendo hicho kwamba ni unyonyaji dhidi yao.

Kutokana na hali hiyo, wameiomba Serikali Kuu kuingilia kati kudhibiti ujazo huo kwa maelezo kuwa halmashauri yao imeshindwa kutatua kuwafanya waendelee kunyonywa na kuwafanya waendelee kuwa maskini.

Wakizungumza na waandishi wa habari katika Kijiji cha Isapulano, walisema wamekuwa wakishindwa kuwakatalia wanunuzi kuendelea na mfumo huo kutokana na hali ya maisha kuwa ngumu.

Felister Salat, alisema wanunuzi hao wamekuwa wakiwatishia kwamba wasipokubaliana na ujazo huo viazi vyao havitanunuliwa, hali ambayo huwalazimisha kukubali kuuza, huku wakijua wanaumia.

"Wanunuzi wanakwambia hawatanunua viazi vyetu bila kujaza lumbesa, sasa unajikuta watoto wanatakiwa kula, kusoma na matumizi mengine muhimu, kwa hiyo tunakubali hivyo hivyo, japo tunaumia sana," alisema Felister.

Naye Heneriko Sanga, alisema wakati wa kulima hakuna mtu anayewasaidia gharama za uzalishaji kwa maelezo kuwa hata kama pembejeo zinauzwa kwa bei ghali hupambana wenyewe, lakini tatizo linaanza baada ya kuvuna.

Alisema wananunua mbolea ambayo ujazo ni ule ule nchi nzima, lakini wanunuzi wa viazi wanataka kununua viazi vyao kwa ujazo wa lumbesa, lakini hakuna ofisa yeyote wa serikali wilayani humo ambaye amekuwa akiwasaidia.

Baadhi ya wanunuzi wa viazi walisema wanaendelea kutumia lumbesa kutokana na biashara ya viazi kuwa ngumu sokoni, hivyo wanatumia ujazo huo kama sehemu ya kuwavutia wateja wanunue haraka kwa maelezo kuwa zao hilo likikaa muda mrefu linaoza.

Mmoja wa wanunuzi hao, Abbas Omary, alisema mbali na kuvutia wateja pia Halmashauri ya Makete imegeuza utaratibu huo kuwa kitega uchumi kwa kuwatoza ushuru maalum kwa ajili ya ujazo huo.

"Tunatoa ushuru wa kawaida wa ununuzi wa mazao, lakini tunatozwa Sh. 1000 kama faini ya lumbesa, sasa hatuoni sababu ya kuacha kuutumia utaratibu huu," alisema Omary.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Makete, Sylivester Mbawala, alikiri kuwa lumbesa imeshapigwa marufuku, ingawa bado inaendelea kutokana na wakulima kuonekana wanaridhika na utaratibu, na kwamba wao wana jukumu la kuwasaidia wazalishe kwa tija.

Alisema endapo wakulima watashirikiana na serikali, kuna uwezekano utaratibu huo ukafika kikomo lakini kwa kuwa wanaridhika ni vigumu kuukomesha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Francis Namaumbo, alikiri kuwatoza tozo za ziada wanunuzi wanaonunua viazi kwa lumbesa, kwa maelezo kuwa lengo sio kuchochea biashara hiyo bali ni sehemu ya mikakati ya kuukomesha.

Alisema fedha hizo zikishakusanywa halmashauri inazirudisha kwa wakulima kwa kuwapelekea miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao.





# Udhalilishaji kijinsia waongezeka Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDADI ya matukio ya udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Juni, mwaka huu, yameongezeka Zanzibar ikilinganishwa na mwezi wa Mei, mwaka huu ambayo yalikuwa 66 na kufikia 97.

Hayo yalielezwa na Ramla Hassan Pandu, kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kitengo cha makosa ya jinai, madai na jinsia wakati akitoa takwimu za mwezi za makosa hayo kwa waandishi wa habari ofisini kwake Mazizini nje kidogo ya mji wa Zanzibar.

Alisema matukio hayo 97 kwa mwezi wa Juni ni 49 kubaka, 11 kulawiti, 21 kuingilia kinyume na maumbile, 10 kutorosha na sita shambulio la aibu.

Alisema matukio hayo kwa mwezi wa Mei yalikuwa 66 ambapo kubaka yalikuwa 43, kulawiti saba, kutorosha saba na shambulio la aibu ni tisa.

Alisema kuwa matukio hayo ya mwezi wa Juni waathirika ni wanawake na watoto na kwamba watoto waliodhalilishwa ni 88 na wanawake ni tisa.

"Matukio kama hayo ya udhalilishaji kwa mwezi wa Juni mwaka jana 2020 yalikuwa 102 ambapo kubaka yalikuwa 38, kulawiti saba, kutorosha saba, shambulio la aibu matano, shambulio 44 na moja kuingilia kinyume na maumbile," alisema Ramla.

Vilevile, alisema kwa mwezi wa Juni mwaka huu, Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja, inaongoza ikilinganishwa na wilaya zingine kwa matukio yaliyoripotiwa wilayani humo ikifuatia na Wilaya ya Mjini Unguja yenye matukio 18.

Alisema hatua zilizochukuliwa matukio 92 yapo chini ya upelelezi wa polisi, matukio matano yapo katika hatua nyingine, manne yapo ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na tukio moja lipo mahakamani.

Katika hatua nyingine Mahakama Kuu ya Zanzibar imemhukumu miaka 30 jela mshtakiwa Hassan Mohammed Ali, mkazi wa Nyerere Unguja, baada ya kutiwa hatiani kwa makosa mawili ya udhalilishaji ikiwamo kutorosha na kubaka.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu wa Mahakama hiyo, Makame Mshamba Simgeni na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Asma Juma, baada ya kuridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka na kumtia hatiani mshtakiwa huyo ili kuwa fundisho kwake na wengine wenye tabia kama hiyo.

Awali, mshtakiwa huyo alidaiwa kutenda makosa hayo Septemba 3, mwaka 2020 majira ya saa 10:00 jioni huko Nyerere na alimtorosha na kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka 14.

Kesi hiyo ilifunguliwa mahakamani hapo Desemba 7, mwaka jana na kuanza kusikilizwa ushahidi Desemba 21 na kutolewa hukumu hiyo wiki iliyopita.

## Wahudumu afya watakiwa kutoa huduma bora

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Uzini, Khamis Hamza Chilo, amewataka madaktari na wahudumu wa afya kutoa huduma zilizo bora licha ya mazingira magumu wanayokutana nayo.

Akizungumza wakati akikabidhi msaada wa vifaa kwa ajili ya vituo mbalimbali vya afya, huko Mwera Wilaya ya Kati Unguja, alisema Jimbo la Uzini bado linahitaji mikakati madhubuti ili wananchi wa jimbo hilo wapate huduma bora za afya.

Alisema madaktari na wahudumu wa afya bado wanakabiliwa na changamoto, ikiwamo uhaba wa vifaa, na kuahidi kuzitafutia ufumbuzi kwa kushirikiana na serikali, wananchi pamoja na viongozi mbalimbali wa jimbo hilo.

"Kupitia ilani ya CCM na viongozi wa Jimbo la Uzini kwa kushirikiana na serikali tutazitatua changamoto hizi kila hali itakaporuhusu," alisema.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado inaendelea na jitihada za kuhakikisha wananchi wote wa Zanzibar wanapatiwa huduma bora za afya nchini na kuwataka wahudumu wa afya kufanya kazi kwa bidii.

Alisema msaada huo wa magodoro na mito wenye thamani ya Sh. 2,275,000 utatumika katika vituo vya afya ambavyo vinahudumia wazazi, kinamama na watoto.

Naye Mwakilishi wa jimbo hilo, Haji Shabani Waziri, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari ya maradhi ya corona ambayo tayari Wizara ya Afya ya Zanzibar imethibitisha kuwapo kwa wagonjwa.

Aidha, aliwataka madaktari kutumia taaluma yao kutoa elimu kwa jamii ili kujikinga na maambukizi ya corona, ikiwa ni pamoja na kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa maji na sabuni na vitakasa mikono na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

Naye Ofisa Tabibu wa Kituo cha Afya Mwera, Dk. Salum Makame, aliushukuru uongozi wa Jimbo la Uzini kwa juhudi wanazozichukua za kuimarisha sekta ya afya katika jimbo hilo.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akitoa agizo kwa viongozi wanaosimamia taasisi mbalimbali kuacha mara moja tabia ya kuwasumbua wawekezaji walioonyesha nia ya kuwekeza Zanzibar, kupitia sekta mbalimbali alipotembelea kiwanda cha maji Chamanangwe. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Aonya tabia ya kuwazungusha wawekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewaagiza watendaji wa taasisi za serikali kuacha mara moja tabia ya kuwazungusha wawekezaji walioonyesha njia ya kuwekeza Zanzibar ili kutoa fursa kwa nchi kupiga hatua za kimaendeleo.

Hemed alisema hayo wakati alipofanya ziara ya kutembelea eneo linalojengwa kiwanda cha kutengeneza maji kinachojengwa katika eneo la Chamanangwe Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema jambo la kuwazungusha wawekezaji walioonyesha nia ya kuwekeza katika ardhi ya Zanzibar halikubaliki na serikali inayoongozwa na Dk. Hussein Mwinyi, haitolifumbia macho kwa kuwa kufanya hivyo kunalenga kurejesha nyuma azma ya serikali ya kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Alisema Zanzibar ilipoteza fursa siku zilizopita kwa kuwasumbua watu wenye nia ya kuwekeza katika maeneo mbalimbali kutokana na watendaji wa taasisi za serikali kuwasababishia usumbufu wawekezaji hao.

"Ni marufuku kwa mtendaji yeyote yule wa taasisi yoyote kuzuiwa masuala ya uwekezaji," alisema.

Hemed alisema, endapo serikali itagundua kuna taasisi inazorotesha kasi ya maendeleo ya serikali ya awamu ya nane, hatua za haraka za kuwaondoa wasimamizi wa taasisi hizo zitachukuliwa.

Alisema kuna faida nyingi zinazopatikana kutokana na uwekezaji huku akitolea mfano kutokana na uwekezaji inaisaidia serikali kukusanya kodi kwa ajili ya uendeshaji wa nchi sambamba na kutoa fursa za ajira kwa vijana.

Aligusia kuwa kuwapo kwa uwekezaji nchini pia kutaisaidia serikali kutatua changamoto za wananchi ikiwamo ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama, uhaba wa dawa pamoja na kukosekana kwa vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika sekta ya elimu.

Naye mwekezaji anayejenga kiwanda hicho Amos Industry Limited, Husamudin Ali Mussa, aliipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa jitihada zake kwa kuwapa kipaumbele wawekezaji kuwekeza jambo ambalo linatia moyo na wawekezaji wengi wameanza kujitokeza.

Alisema, kiwanda hicho kitakapokamilika kitaanza uwekezaji wake kwa kutengeneza maji ya kunywa, lakini baada ya muda mfupi kitajikita katika utengenezaji wa juisi za matunda na malengo ya baadaye wamekusudia kuanzisha kiwanda cha kutengeneza mabati hatua itakayowapunguzia wananchi wake gharama ya upatikanaji wa bidhaa mbalimbali.

Husamudin alimwambia Makamu wa Pili wa Rais, ujenzi wa kiwanda hicho unaoendelea sasa unatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi mitatu huku wakiwa tayari wameshaagiza vifaa kwa ajili ya kufanya kazi katika kiwanda hicho.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Sharif Ali Sharif, alisema kukamilika kwa kiwanda hicho kutasaidia kwa kiasi kikubwa kufikiwa kwa utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kufikia lengo la kutoa ajira 300,000 kwa vijana wa Zanzibar.

Sharif alimwomba Makamu wa Pili wa Rais kupitia serikali kuangalia namna bora ya kulinda soko la ndani kwa wawekezaji walioamua kuwekeza Zanzibar kwa kuwa muda mrefu kumekuwa na changamoto ya ushindani wa soko kwa waingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAPANGISHWA

NYUMBA INAPANGISHWA INA VYUMBA VINNE KIMOJA MASTER BEDROOM, IPO MAENEO YA MWENGE NZASA, INA MAJI NA UMEME ,IPO NDANI YA FENCE(UKUTA)

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**PIGA SIMU NAMBA:0682 600 101**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.221/2021**

Ombi la **ADAM MEDARD MSIMBE** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **RUKIA KOSA LALI**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **23/08/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 19/07/2021**

*116364502*

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JUMA SHAIBU JUMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **BESTA PASCHAL KALUMNA** aina ya **TVS - STAR** yenye namba za usajili **MC 140 CKF** .Chasis **No.MD625AF78K1001139, Engine No. AF7CK1301118.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/355067/2021.**

*116364402*

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MJIBU RUFAA**
**(MCA/84)**
**MAHAKAMA YA WILAYA DODOMA**
**RUFAA JINAI NAMBARI 25/2021**
**MLETA RUFAA SILVIA CHAWE**
**MJIBU RUFAA: SALUTWA EMMANUEL**
**Kwa kuwa mleta Rufaa ameleta maombi yake kwamba**
**MAOMBI YA KUKATA RUFAA**

Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya **IJUMAA Tarehe 30/7/2021** saa 2.00 asubuhi kwa kujibu maombi hayo.
Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo **tarehe 9/7/2021**.

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT
Hakimu Mkazi
DODOMA

*116364702*

---

## PUBLIC ANNOUNCEMENT TO CLOSE THE COMPANY

THE SHAREHOLDERS OF BELFORD INVESTMENT LIMITED (REGISTRATION NO 68716 DATED 26TH NOVEMBER 2002 IN ACCORDANCE WITH THE COMPANIES LAWS AT BRELA WISH TO SHUT DOWN THE COMPANY OPERATION DUE TO CIRCUMSTANCES THAT ARE BEYOND OUR CAPABILITY.

*116364802*

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Mahakama ya wilaya ya DODOMA MJINI**
**Wilaya ya DODOMA**
**MADAI NAMBARI 88/2021**
**MDAI DIANA URIO**
**MDAIWA GABRIEL KIMARO**
**Kwa GABRIEL KIMARO**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TSH 700,000/=**

Hivyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya Tarehe 23/07/2021 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea shauri hilo.
Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama itadhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakamahii leo tarehe 16/07/2021.

*116365102*

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LINUS LEONARD JOSEPH** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **NOAH** yenye namba za usajili **T457 DCB** Lenye chassis namba **SR400280699** Engine no **3S2867933** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/474251/2019**

*116365202*

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OSCAR WILSON KILASI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISH CANTER** yenye namba za usajili **T894 CSV** Lenye chassis namba **FE325E560990.** Engine no **4D32A13492.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/355620/2021.**

*116365802*

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

---

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## TANGAZO

# MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

MCB BANK BETTER TOGETHER

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

| WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2021 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 30-Juni-2021 | Robo Mwaka iliyopita 31-Machi-2021 |
|---|---|---|
| **A. MALI:** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 494 | 786 |
| 2. Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 2,369 | 2,926 |
| 3. Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4. Salio katika Benki nyingine na Taasisi za fedha | 41 | 39 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | 181 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | - | 202 |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 2,300 | 5,000 |
| 10. Uwekezaji katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 36,142 | 28,163 |
| 12. Mali Nyingine | 4,531 | 5,143 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 896 | 846 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **46,773** | **43,286** |
| **B. DHIMA:** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18. Amana za Wateja | 27,832 | 24,036 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20. Amana Maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 880 | 819 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 90 | 145 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | 280 | 341 |
| 27. Dhima Nyingine | 1,637 | 1,488 |
| 28. Madeni | - | - |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | **30,719** | **26,829** |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI** | **16,054** | **16,457** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA:** | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 30,912 | 30,912 |
| 32. Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (18,507) | (18,507) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (1,351) | (948) |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji (Mtaji tangulizi) | 5,000 | 5,000 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **16,054** | **16,457** |
| **38. DHIMA ZISIZO DHAHIRI** | | |
| 39. Mikopo Chechefu | 346 | 273 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | (309) | (330) |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| - Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 34% | 38% |
| - Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.9% | 1.0% |
| - Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 129% | 116% |
| - Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 77% | 64% |
| - Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 82% | 77% |
| - Ongezeko la Amana | 16% | 30% |
| - Ongezeko la Mali | 8% | 12% |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2021 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo ya Mwaka sasa 30-Juni-2021 | Robo ya mwaka Linganishi 31-Machi-2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Juni-2021 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Juni-2020 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 1,243 | 646 | 2,255 | 1,319 |
| 2. Gharama za Riba | 382 | 99 | 706 | 222 |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **861** | **547** | **1,549** | **1,097** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (21) | (25) | (21) | (25) |
| 6. Mapata Yasiyo ya Riba: | 187 | 60 | 279 | 121 |
| 6.1 Faida (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za kigeni | 1 | 3 | 1 | 6 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 184 | 56 | 278 | 112 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 2 | 1 | - | 3 |
| 7. Gharama Zisizo za Riba | 1,472 | 1,607 | 3,200 | 3,170 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 697 | 697 | 1,429 | 1,359 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 775 | 910 | 1,771 | 1,811 |
| **8. Faida (Hasara) ya Uendeshaji** | **(403)** | **(975)** | **(1,351)** | **(1,927)** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| **10. Faida (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **(403)** | **(975)** | **(1,351)** | **(1,927)** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(403)** | **(975)** | **(1,351)** | **(1,927)** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 53 | 61 | 53 | 61 |
| 14. Mapato kwa Hisa | -7 | -16 | -22 | -31 |
| 15. Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| - Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | *-1%* | *-4%* | *-3%* | *-7%* |
| - Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | *-2%* | *-7%* | *-8%* | *-13%* |
| - Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | *140%* | *265%* | *175%* | *260%* |
| - Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | *2%* | *3%* | *4%* | *7%* |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI 2021 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 30-Juni-2021 | Robo Mwaka iliyopita 31-Machi-2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Juni-2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Juni-2020 |
|---|---|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato (Hasara) Halisi | (403) | (948) | (1,351) | (1,927) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| - Hasara katika Mali | 343 | 346 | 689 | 614 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (5,279) | (5,766) | (11,045) | 805 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 6,996 | 5,511 | 12,507 | (2,147) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 296 | (242) | 54 | (16) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 100 | (802) | (702) | 991 |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **2,054** | **(1,902)** | **152** | **(1,680)** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - |
| - Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Mali za Kudumu | (120) | - | (120) | (12) |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(120)** | **-** | **(120)** | **(12)** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | - | - | - | - |
| - Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| - Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| - Mengineyo (Mtaji tangulizi) | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - | - | - |
| - Ongezeko / Punguzo Halisi katika Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu | 1,933 | (1,902) | 32 | (1,692) |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 2,958 | 4,859 | 4,485 | 4,274 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 4,891 | 2,958 | 4,516 | 2,582 |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2021 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Mtaji tangulizi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (18,507) | - | - | 12,405 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (1,351) | - | - | (1,351) |
| Mtaji tangulizi | - | - | - | 5,000 | 5,000 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(19,858)** | **-** | **5,000** | **16,054** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (14,445) | - | - | 16,467 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (4,062) | - | - | (4,062) |
| Mtaji tangulizi | - | - | - | 5,000 | 5,000 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(18,507)** | **-** | **5,000** | **17,405** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2021

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha za robo, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| Richard L. Makungwa (Ofisa Mtendaji Mkuu) | ......................... (Imesainiwa) | 16 Julai 2021 |
| Selemani Kijori (Mkuu wa Fedha) | ......................... (Imesainiwa) | 16 Julai 2021 |
| Patrick Mashalla (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | ......................... (Imesainiwa) | 16 Julai 2021 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| *Jina* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| 1/ Francis Ramadhani (Mwenyekiti wa Bodi) | ......................... (Imesainiwa) | 16 Julai 2021 |
| 2/ Celestin Muganga (Mkurugenzi wa Bodi) | ......................... (Imesainiwa) | 16 Julai 2021 |

## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES MADE UNDER REGULATION 11

| S/N. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1 | Current Accounts | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 50,000 |
| | (b) Monthly service fee (breakdown per customer type) | TZS 7,500 |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS 2,500 for amounts less than 5Mil otherwise 0.1% max TZS 100,000 |
| | (d) Fees per ATM withdrawal | TZS 1,300 |
| | (e) ATM mini statement | TZS 300 |
| | (f) Interim statement per page | TZS 1,500 |
| | (g) Periodic scheduled statement | 0 |
| | (h) Cheque book | TZS 500 per leaf |
| | (i) Dishonoured cheque | TZS 100,000 |
| | (j) Special clearance | n/a |
| | (k) Counter cheque | TZS 6,000 |
| | (l) Stop payment | TZS 40,000 |
| | (m) Standing order (Same bank) | Free |
| | (n) Balance enquiry | TZS 300 |
| | (o) New ATM card issuance | TZS 10,000 |
| | (p) ATM card renewal or replacement (indicate costs for different card types) | TZS 10,000 |
| | (q) Overdrawn account interest charge | 20% |
| | (r) Unarranged overdraft | 20% |
| | (s) Interbank transfer | TZS 10,000 |
| | (t) Bill payments through ATM | n/a |
| | (u) Deposit fee | 0 |
| | (v) Other (please specify) | n/a |
| 2 | Savings Accounts (Disclose for product specific types) | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 5,000 |
| | (b) Monthly service fee | TZS 1,400 |
| | (c) Interim statement | TZS 1,500 |
| | (d) Account closure | TZS 20,000 |
| 3 | Electronic Banking | |
| | (a) Internet banking monthly fee | n/a |
| | (b) Internet transfers | n/a |
| | (c) SMS banking | TZS 1700 |
| | (d) Other | n/a |
| 4 | Foreign Exchange Transaction | |
| | (a) Purchase/sale of TCs transactions over the | n/a |
| | (b) Purchase of foreign cheque | n/a |
| | (c) Sale/purchase of cash passport | n/a |
| | (d) Telegraphic transfer | n/a |
| | (e) Telex/SWIFT | n/a |
| | (f) Tranfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank) | 0 |
| 5 | Personal Loans | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | 1.77% p.a |
| | (i) Personal loans | 16% |
| | (ii) Overdrafts | 20% |
| | (iii) Mortgage finance | n/a |
| | (iv) Asset finance | n/a |
| | (b) Unpaid loan instalment | 20% |
| | (d) Valuation fees | n/a |
| | (e) Other | n/a |

Deposit Rates

| Fixed Deposit - TZS | 3 Months | 6 Months | 12 Months |
|---|---|---|---|
| 1 - 2 Mln | 1.5% | 2.0% | 2.5% |
| 2 - 10Mln | 2.0% | 2.5% | 3.0% |
| 10 - 50 Mln | 2.5% | 3.0% | 3.5% |
| 50 - 100 Mln | 3.0% | 3.5% | 4.0% |
| 100 - 300 Mln | 3.5% | 4.0% | 4.5% |
| 300 - 500 Mln | 4.0% | 4.5% | 5.0% |
| 500m - 1Bln | 4.5% | 5.0% | 5.5% |
| Above 1 Bln | Contact Treasury | | |

| Savings Account - TZS | Accrue on Daily Cleared balance paid Monthly |
|---|---|
| 0- 50k | 0.5% |
| 50k - 1mln | 1.0% |
| 1 - 10mln | 1.5% |
| 10 - 100mln | 2.0% |
| Over 1mln | 2.5% |

Base Lending Rates

| | Loan Type | Base rate | |
|---|---|---|---|
| 1 | Short term (up to 1year | 19.5% | +/-4.5% |
| 2 | Medium term (2-4 years | 21.5% | +/-1.5% |
| 4 | Term loans (over 5 year | 19.0% | +/-4.0% |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Richard L. Makungwa | Chief Executive Officer | | 16 July 2021 |
| 2 | Leticia Ndongole | Head of Business Development & Marketing | | 16 July 2021 |
| 3 | Selemani Kijori | Head of Finance | | 16 July 2021 |




MCB BANK

VISA

0800 750 033 @mwalimubank

**Head Office**
Mlimani Tower - Mezzanine Floor,
Sam Nujoma Road
Phone: 022-2772954/7
email: info@mcb.co.tz
Customer Care No.:
0629331151|0629331755|080 0750033

**Mlimani Branch**
Mlimani Tower - Ground Floor
Sam Nujoma Road
P.O.Box 61002,
Dar es salaam

**Samora Branch**
Samora Avenue
Consolidated Holding Building Ground Floor

**Regional Office - Morogoro**
19, Plot E, Nkomo Street
Phone: +255 622 005 574
Morogoro

**Regional Office - Mbeya**
90, Plot L, Sokomatola Street
Phone: +255 766 903 575
Mbeya

**Regional Office - Mwanza**
18, Plot A, Kirumba Street
Phone: +55 788 138 238
Mwanza

216366202




# SOLSKJAER:
## Lingard yupo kwenye mipango yangu

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amedai Jesse Lingard yupo kwenye mipango ya timu hiyo kuelekea msimu wa 2021/2022.

Kauli hiyo ya Solskjaer imekuja katika mechi ya kwanza ya kirafiki kati ya Manchester United na Derby County ambapo Lingard aliingia kutokea benchi na kuonyesha kiwango cha kuvutia.

Solskjaer alieleza kuwa Lingard ni mchezaji mzuri na alipokuwa kwenye mkopo aliweza kujitathmini na sasa amerejea akiwa imara zaidi na yupo tayari kumfanya chaguo lake kuelekea msimu ujao.

Lingard alienda West Ham United kwa mkopo wa muda mfupi na kuonyesha kiwango kizuri kwa kufunga mabao nane, huku akivutia macho ya timu mbalimbali huku wagonga nyundo hao wa London wakitaka kumsajili moja kwa moja.

Nyota huyo wa England sasa ana nafasi ya kuwa kwenye kikosi cha kwanza cha United, baada ya Marcus Rashford kufanyiwa upasuaji wa bega ambalo litamweka nje ya dimba kwa kipindi cha miezi miwili hadi mitatu.

Katika mechi hiyo Solskjaer pia alikutana na Wayne Rooney ambaye aliwahi kucheza naye United na matokeo katika mechi hiyo ilikuwa ni ushindi wa magoli 2-1, huku makinda wa United wakitupia magoli yote mawili.

# CHELSEA YAMTENGEA KITITA LEWANDOWSKI

**LONDON, England**

KWA mujibu wa ripoti ya gazeti la The Sun, Klabu ya Chelsea wanaandaa mipango ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Poland na Bayern Munich, Robert Lewandowski katika dirisha hili la majira ya joto.

Chelsea wamehamishia silaha zao kwa Lewandowski mwenye umri wa miaka 32 baada ya kushindwa katika juhudi zao za kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland ambaye atasalia katika klabu yake.

Chelsea wanatarajia kuandaa dau lenye thamani ya pauni milioni 50 kwa ajili ya kuishawishi Bayern Munich kumuuza mchezaji huyo.



Lewandowski ana mkataba na Bayern hadi mwaka 2023 na mabingwa hao wa Ujerumani wanasita kumruhusu aondoke, lakini dau la pauni milioni 50 linaweza kufanya wabadili mawazo yao.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Dortmund anasemekana ana hamu ya kucheza katika Ligi Kuu England na angefurahi kuhamia kwa miamba hao wa London Magharibi.

Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel anamtaka straika huyo na ana imani ayaweza kufiti kwenye kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao.

Lewandowski msimu uliopita ulikuwa wa kuvutia sana kwake, kwani alifunga mabao 41 kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga na kujiweka rekodi yake.

# United njia nyeupe kumnasa Vinicius

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imetajwa kuwa wamepewa nafasi ya kumsajili Vinicius Junior wa Real Madrid.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 21 alikuwa na msimu wa kawaida pale kwa Los Blancos katika msimu wa 2020-21, akicheza mechi 49 kwenye mashindano yote.

Lakini raia huyo wa Brazil anadaiwa kuwapo sokoni msimu huu wa majira ya joto, kwani Real Madrid wanataka kuweka sawa vitabu vyao vya fedha kabla ya uwezekano wa kukamilisha uhamisho wa nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe.

United na Real Madrid tayari wametajwa kuwapo kwenye mazungumzo juu ya Raphael Varane, lakini kwa mujibu wa The Mirror, mabingwa hao mara 20 wa Ligi Kuu England pia wamepewa nafasi ya kumsajili Vinicius.

Ripoti hiyo inadai kwamba kikosi hicho cha Carlo Ancelotti kinataka pauni milioni 68.5, lakini Mashetani Wekundu wanaweza kumsaini kwa mkopo kwa 2021-22 na uwezekano wa makubaliano ya kudumu mwaka ujao.

United inayonolewa na Ole Gunnar Solskjaer inadaiwa imeweka wazi kuwa wanavutiwa na mshambuliaji huyo, ambaye amefunga mara 14 na kusajili asisti 23 kwenye mechi 118 za Real Madrid.



## HABARI MICHEZO

# Diaz kusaini mkataba Milan

**MILAN, Italia**

SASA ni suala la muda tu kabla ya tangazo rasmi kwamba, Brahim Diaz anasaini mkataba mpya na klabu ya AC Milan.

Mshambuliaji huyo wa Real Madrid aliwasili hapo kwenye dimba la San Siro kwa mkopo wa miaka miwili wenye thamani ya uero milioni 3 na kipengele cha kumnunua moja kwa moja kwa pauni milioni 22 ifikapo Juni 2023.

Calciomercato.com inaripoti kuwa Los Blancos wana kifungu cha kumnunua katika dili hilo kwa thamani ya euro milioni 27, sababu Diaz anarudi Rossoneri kwa angalau miaka miwili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye alihamia Real Madrid kutoka Manchester City Januari 2019, alitumia msimu wa 2020-21 kwa mkopo na Diavolo, wakati Milan wakimaliza katika nafasi ya pili kwenye Serie A.

Diaz alicheza michezo 39 ya mashindano yote msimu wa 2020-21, akichangia mabao saba na asisti nne katika mchakato huo.





# SIMEONE
## aitaka Atletico kumsajili Aarons

**MADRID, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Atletico Madrid, Diego Simeone, amewaambia viongozi wa klabu hiyo wamsajili mlinzi wa Norwich, Max Aarons kama mbadala wa Kieran Trippier endapo ataondoka.

Trippier anaripotiwa huenda akaondoka Atletico Madrid majira haya ya joto ili kujiunga na Manchester United yenye makazi yake kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Na Simeone anaona kwamba, Aarons ndiye anayefiti kuchukua mikoba ya mlinzi huyo wa kimataifa wa England.

Kwa mujibu wa ripoti ya Mail, Aarons thamani yake ni zaidi ya pauli milioni 28 na klabu inayomtaka inatakiwa kufikia kiasi hicho.

Awali Arsenal na Chelsea zilikuwa zikihusishwa kuwania saini ya nyota huyo wa kimataifa wa England.

Inaamini kwamba, Atletico Madrid wazaweza kutoa pauni milioni 25 kwa mlinzi huyo wa kushoto ambapo Simeone anatajwa kuwa ni shabiki yake mkubwa.

Aarons amecheza mechi 42 na kuhusika kwenye mabao matano kwa timu hiyo msimu uliopita, huku pia akihusishwa na Everton, West Ham na Tottenham Hotspur.



# Pogba atakiwa kustaafia United

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United inataka Paul Pogba abaki Old Trafford hadi pale atakapoamua kustaafu kama mchezaji, kwa mujibu wa ripoti za magazeti ya Ulaya.

Nyota huyo zamani wa Juventus sasa amebakiza miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake na Mashetani Wekundu, na uvumi juu ya hatima yake majira haya ya joto unaendelea kubamba kuwa anaondoka klabuni hapo.

Paris Saint-Germain inadhaniwa kuwa inaweka mipango ya uhamisho wa pauni milioni 51 kwa ajili ya Pogba, wakati United ikitajwa kumleta Eduardo Camavinga kama mbadala wake.

Lakini kwa mujibu wa The Athletic, kikosi cha kocha Ole Gunnar Solskjaer bado kina matumaini kuwa kiungo huyo anaweza kusaini mkataba mpya wa muda mrefu, ambao utamfanya abaki klabuni hadi atakapotundika daluga zake za soka.

Ripoti hiyo imeongeza kuwa Pogba hataki sana kuhamia PSG na atakuwa tayari kusaini makubaliano mapya huko United, licha ya madai ya wakala wake, Mino Raiola ya mwaka jana kwamba, wakati wa mteja wake kuwa na Mashetani Wekundu ulikuwa "umekwisha".

Pogba alifunga bao moja na kusaidia moja zaidi akiwa na Ufaransa wakati wa michuano ya Euro 2020, na ameandika rekodi ya mabao 38 na pasi za mwisho 42 kwenye mechi 206 akiwa na United.

## KWA UFUPI

### INTER YAMTAKA DUMFRIES

INTER Milan inataka kumsajili beki wa PSV Eindhoven, Denzel Dumfries mwenye umri wa miaka 25, lakini inaweza kumnunua kwa mkopo mchezaji huyo wa Uholanzi. ***(Calciomercato)***

### NIGUEZ ATAJWA LIVERPOOL

HAKUNA habari yoyote mpya kuhusu uhamisho wa Saul Niguez kutoka Atletico Madrid kuelekea Barcelona na kiungo huyo wa Hispania (26), amekuwa akiwasiliana na klabu kadhaa, huku akitarajiwa kujiunga na Liverpool au Manchester United ***(AS)***

### CHELSEA YAKOMAA NA HAALAND

CHELSEA inajaribu kufanya kila kitu katika harakati zake za kumwania mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20. ***(Sky Germany)***

### HUDSON-ODOI KUONDOKA

CHELSEA pia imepanga kumbadilisha winga wa England, Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 20 na Kingsley Coman wa Bayern Munich katika mpango wa kubadilishana wachezaji. ***(L'Equipe)***

### ARSENAL YAMTAKA AARONS

ARSENAL imeingia katika harakati za kumsajili beki wa Norwich na England mwenye umri wa miaka 21, Max Aarons - huku washikabunduki wakiwa katika mpango wa kutaka mchezaji atakayechukua nafasi ya Hector Bellerin mwenye umri wa miaka 26. ***(Express)***

### EVERTON KUMSAJILI TOWNSEND

EVERTON inakaribia kumsajili winga wa England, Andros Townsend mwenye umri wa miaka 30, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Crystal Palace na atakuwa mchezaji wa kwanza kusajiliwa na kocha mpya, Rafael Benitez , Klabu hiyo pia inamsaka winga wa klabu ya Bayer Leverkusen na England Demarai Gray mwenye umri wa miaka 25. ***(Mirror)***

### EVERTON YAMTAKA LENGLET

EVERTON pia ni mojawapo ya klabu mbili pamoja na wapinzani wao katika Ligi Kuu England, West Ham, kuwasiliana na Barcelona kuhusu makubaliano ya kumsajili beki wa Timu ya Taifa Ufaransa mwenye umri wa miaka 26, Clement Lenglet. ***(AS)***

### JUVE KUMSAJILI JESUS

JUVENTUS italazimika kulipa pauni milioni 43 ili kumpata mashambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Gabriel Jesus kutoka Manchester City. ***(Calciomercato)***

### PAREDES AINGIA SOKONI

JUVENTUS pia inafikiria kumnunua kwa mkopo kiungo wa kati wa Argentina, Leandro Paredes mwenye umri wa miaka 27 ili kuziba pengo la mchezaji wa Brazil, Authur Melo mwenye umri wa 24 ambaye ni majeruhi. ***(La Repubblica via Football Italia)***

### BARCA YAMTAKA SANCHEZ

BARCELONA ina hamu ya kumsajili kiungo wa kati wa Lille na Ureno, Renato Sanches kwa mkopo wakiwa na fursa ya kumnunua. Mchezaji huyo mwdenye umri wa miaka 23 ana thamani ya pauni milioni 30, dau ambalo Barcelona haiwezi kuafikia ili kumnunua. ***(AS )***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL HATIHATI KUMNASA LOCATELLI

**Ni baada ya Juve kuongeza nguvu kwenye mbio za kumsajili kiungo huyo wa...**

**LONDON, England**

JUVENTUS ipo tayari kuipiku Arsenal kwenye mbio za kuwania kumsajili nyota anayewindwa sana kwa sasa, Manuel Locatelli, kwa mujibu wa The Guardian.

Kiungo huyo anayeichezea Sassuolo inayoshiriki Ligi Kuu Italia (Serie A), aling'ara zaidi kwenye michuano ya Euro 2020 iliyomalizika wiki iliyopita.

Baada ya michuano hiyo, Locatelli mwenye umri wa miaka 23 amekuwa akiwaniwa na klabu kadhaa kubwa za Ulaya kwa ajili ya kuhitaji huduma yake kuelekea msimu mpya wa ligi mbalimbali za Ulaya.

Arsenal ilikuwa timu ya kwanza kuonyesha nia ya kutaka kumsajili Locatelli baada ya kuisaidia Italia kutwaa taji la Euro 2020, walishatuma viongozi wao kwa ajili ya kuonana na wawakilishi wa mchezaji huyo.

Lakini sasa kwa mujibu wa ripoti ya jana, Juventus nao wametia mguu kwa ajili ya kuwania saini ya nyota huyo.

Juventus wanaonekana kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuipiku Arsenal kwenye mbio hizo, kwa sababu Locatelli mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2021-22.

Arsenal walimaliza nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu England na hivyo hawapo kwenye michuano ya Ulaya ikiwa ni kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1996.

Ripoti ya Calciomercato imebainisha kwamba, klabu ya Sassuolo ipo tayari kumuuza nyota wake ili kutafuta fedha za kusajili nyota wengine.

Sassuolo imeripotiwa kutaka euro milioni 40 ili kumwachia Locatelli na Juventus haraka wametuma ofa yake wa ajili ya kumsajili nyota huyo.

Sky Sports Italia imeripoti kuwa Juventus tayari wamepeleka ofa ya euro milioni 30 ambayo imekatakiwa na Sassuolo, inayosisitiza kiasi cha euro milioni 40 ndizo zinazoweza kuwashawishi kumuuza.

Arsenal bado haijatoa ofa yao, lakini sasa inaonyesha wazi kuwa wanaoweza kunyoosha mikono ya kumsajili Locatelli baada ya Juventus kutoa ofa yao na kuna uwezekano wakaiongoza kufikia ile inayotakiwa.

# Kakolanya afurahia ubingwa Msimbazi

Na Shufaa Lyimo

MLINDA mlango wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba Beno Kakolanya amesema licha ya kucheza michezo michache msimu huu anashukuru timu yake imefanikiwa kutwaa ubingwa wa ligi hiyo kwa mara ya nne mfululizo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Kakolanya alisema siri kubwa ya mafanikio ya kikosi chao ilitokana na umoja na ushirikiano waliokuwa nao wachezaji, viongozi na wanachama wa timu hiyo.

"Siri ya mafanikio yetu ni ushirikiano tuliokuwa nao sisi wachezaji, tulishirikiana na benchi letu la ufundi nina imani tutaendeleza ushindani wetu katika mchezo ujao wa fainali ya Kombe la FA ambao utatukunanisha na watani zetu Yanga," alisema Kakolanya.

Aliongeza kwa sasa timu yao inaendelea kujipanga kuhakikisha inapata matokeo mazuri katika mchezo huo utakaochezwa Julai 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika na kukamilisha msimu kwa furaha.

Aliongeza ni wazi mchezo huo unatarajiwa kuwa na ushindani lakini wamejiimarisha kuhakikisha hawapotezi tena mechi dhidi ya Yanga kama ilivyokuwa kwenye mchezo wa marudiano wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Kwa sasa tunajipanga kwa ajili ya kukutana tena na Yanga kwenye fainali ya Kombe la FA, ninaimani hakuna kitakachoshindikana kwa kuwa tumeongeza umakini na kusikiliza maelekezo ya mwalimu wetu, tunaomba mashabiki wazidi kutuombea," Kakolanya alisema.

Simba itashuka katika mechi hiyo ikiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0 katika mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Julai 3, mwaka huu.

# Mtibwa Sugar: Hatushuki daraja

Na Saada Akida

BAADA ya kunusurika kushuka daraja, uongozi wa Mtibwa Sugar umesema umeshafahamu mahali walipokosea, hivyo wataingia kupambana kuhakikisha wanaibakiza timu yao katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mtibwa Sugar itakutana na Transit Camp katika mechi ya mchujo itakayochezwa kesho na marudiano yakipangwa kufanyika Julai 24, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Mohammed Badru alisema malengo makubwa waliyonayo ni kupata ushindi katika mechi ya kwanza ili kujiweka kwenye mazingira salama ya kumalizika kazi watakaporudiana.

Badru alisema kwa sasa wanapambana kuhakikisha hawaichezea nafasi iliyobakia ya kujinusuru, kwenye michezo hiyo miwili iliyobakia.

"Tumemaliza ligi na kupata nafasi ya kucheza mechi za 'play off', hii nafasi yetu ya kipekee ambayo tunahitaji kuitumia vizuri na kupata ushindi ili kufikia malengo yetu ya timu kubakia."

Nina imani na wachezaji wangu watahakikisha tunafanya vizuri katika mechi hizo za 'Play Off', tumejipanga kikamilifu kwa hatua hiyo muhimu na ngumu," alisema Badru.

Timu nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyoangukia kwenye 'kapu' la mchujo ni Coastal Union ambayo itacheza dhidi ya Pamba ya jijini Mwanza.

# MWINYI AISHUKURU NMB, AFUNGUKA KUHUSU RIADHA

Na Mwandishi Wetu

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ambaye aliongoza katika mbio za kilomita tano za 'NMB 5K Run 2021,' amesema mashindano hayo ya marathoni yatakuwa ni chachu ya kuibua na kuendeleza vipaji vya wanariadha ambayo baadaye vitaitangaza Zanzibar kimataifa.

Akizungumza kabla ya kukabidhi medali na zawadi kwa washindi wa mbio za kilomita tano, 10, 21, watoto, wenye ulemavu na wagonjwa wa afya ya akili walioshiriki mbio hizo, Rais Mwinyi aliwashukuru waratibu, lakini akawapongeza wadhamini, wakiwamo NMB kwa kuzirejesha mbio hizo zilizofanyika kwa mara ya mwisho miaka 10 iliyopita.

Alisema waratibu na wadhamini wameonyesha dhamira ya dhati ya kushirikiana na serikali yake katika kukuza uchumi, kuhamasisha utalii na kuhimiza mazoezi ya viungo.

"Serikali inaahidi kuwa mashindano haya yatafanyika kila mwaka kuanzia sasa, ili Zanzibar iweze kupata wakimbiaji mahiri, huku tukiyatumia kama chachu ya kuhamasisha kukuza Uchumi wa Bluu, utalii na kuimarisha afya. Wito wangu kwa wadau ni kuanzisha mbio nyingi zaidi na kudhamini pia michezo mingine," alisema Mwinyi.

Kwa upande wake, Benedicto Baragomwa, ambaye ni Kaimu Ofisa Mkuu Ukaguzi wa Ndani wa NMB, alisema benki yake inajisikia fahari kudhamini mbio hizo na kutokana na NMB kuwa mdau mkubwa wa maendeleo, haikuwa ngumu kwao kufanya uamuzi wa kujitosa katika Zanzibar International Marathon.

"Sisi ni wadau wa maendeleo, na tukavutiwa na malengo ya uwepo wa mashindano haya, tukakubali kudhamini ili kuwa sehemu ya washiriki wa mchakato wa kukuza uchumi wa bluu, utalii na kuimarisha afya za Wazanzibar kupitia michezo.

"NMB tunaahidi kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila hatua inayolenga kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya Taifa," alisema Baragomwa, ambaye alikimbia mbio za kilomita tano.

Katika mbio hizo, Inyasi Nicodemus wa Arusha aliibuka mshindi wa kwanza wa NMB 5K Run 2021 upande wa wanaume, akifuatiwa na Sylvester Naali na Emmanuel Gadiye (wote wa Polisi), huku kinara upande wa wanawake, Aisha Luvuma wa Arusha aliibuka mshindi, Valentina Michael (Arusha) na Catherine Lange (wa Mafunzo) wakimaliza nafasi ya pili na tatu.Mbio za kilomita tano zilikuwa ni sehemu ya mbio za kimataifa za Zanzibar na zilifanyika chini ya kauli mbiu ya 'Tunakuza Uchumi wa Bluu Kupitia Michezo Zanzibar, zilizoanzia eneo la Ngome Kongwe na kumalizikia kwenye Uwanja wa Amaan.

NMB ilitoa kiasi cha Sh. milioni 35, na lengo likiwa ni kuunga mkono jitihada za Serikali ya Zanzibar katika kuhamasisha na kukuza utalii, kukuza Uchumi wa Bluu na kuchagiza jamii kudumisha utamaduni chanya wa kufanya mazoezi ili kuepukana na magonjwa yasiyoambukizwa.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' (kulia), akiwa na mshambuliaji mpya wa timu hiyo, Rogders Kola kutoka Zanaco ya Zambia baada ya nyota huyo kusaini mkataba wa kuwatumikia wenyeji hao wa Azam Complex jijini Dar es Salaam. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Bocco awafuta machozi Wabongo

Na Adam Fungamwango

STRAIKA na nahodha wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, John Bocco ambaye Jumapili iliyopita aliibuka kuwa Mfungaji Bora msimu huu, na kumaliza ufalme wa wachazeji wa kigeni kutwaa kiatu hicho kwa misimu mitatu mfululizo.

Bocco alifunga bao dakika za nyongeza kwa mkwaju wa penalti kwenye mechi kati ya Simba dhidi ya Namungo, Uwanja wa Benjamin Mkapa na kufikisha jumla ya mabao 16 na kurudisha kiatu cha ufungaji bora kwa Watanzania ambayo walionekana kama ni watumwa mbele ya nchi yao.

Mara ya mwisho kwa mchezaji wa Kitanzania kuibuka kuwa mfungaji bora, ilikuwa msimu wa 2016/17, wakati winga wa Yanga wakati huo, Simon Msuva na Abdulrahman Mussa kutoka Ruvu Shooting wapomaliza kuwa vinara wa mabao kwenye ligi hiyo kwa pamoja, walipofunga mabao 14 kila mmoja.

Hii ni mara ya pili kwa Bocco kuwa mfungaji bora kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, maana pia katika msimu wa 2011/12, akiwa Azam FC, alipachika mabao 19 na kutwaa kiatu hicho. Haikuwa rahisi kwa Wabongo kuumaliza ufalme huo, kwani ilibidi wasubiri hadi dakika za mwisho kwani Bocco alikuwa anafungana mabao na Chris Mugalu, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, aliyepachika mabao 15, Mzimbabwe Prince Dube wa Azam FC aliyefunga mabao 14, na Mnyarwanda Meddie Kagere aliyepachika wavuni magoli 13.

Baada ya kina Msuva kutwaa ufungaji bora ilikuja misimu minne ya wafungaji bora wa kigeni kwa 2017/18, Mganda Emmanuel Okwi alitwaa kiatu akiwa na mabao 20, Kagere akitwaa mara mbili mfululizo msimu wa 2018/19 kwa mabao 23 na 2019/20 akiwa na mabao 22.

# Michezo

Jumanne Julai 20, 2021

Nipashe




ARSENAL HATIHATI KUMNASA LOCATELLI HABARI UK 22



Wachezaji wa Simba wakiwa wamembeba juu kocha wao, Didier Gomes, baada ya kumaliza mechi ya mwisho ya msimu wa Ligi Kuu Bara 2020/21 dhidi ya Namungo FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 4-0. PICHA: JUMANNE JUMA

## YANGA YAFUNGUKA SARE ZILIWAMALIZA

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Yanga kimerejea salama jijini Dar es Salam jana kikitokea Dodoma katika mechi ya mwisho ya Ligi Kuu Tanzania Bara huku ikisema matokeo ya sare waliyopata katika baadhi ya mechi zao ndio sababu kuu ya wao kushindwa kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli alisema kikosi chao kimeingia kambini moja kwa moja ili kuendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea mechi yao ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Simba itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Bumbuli alisema kuna makosa yalifanyika katika mechi hizo ambayo yaliwaondoa kwenye mbio za ubingwa wa msimu uliomalizika hasa kwenye mechi za mzunguko wa kwanza.

"Tumerejea leo (jana) na tumeelekea kambini kwa ajili ya mchezo wetu wa fainali dhidi ya Simba, huo ndiyo utakuwa mchezo wetu wa mwisho msimu huu," alisema Bumbuli.

"Kuna makosa yalifanyika ndiyo yaliyosababisha tukose ubingwa, lakini yote kwa yote, sisi tumeyaacha, tunasonga mbele. Kama kauli mbiu yetu inavyosema, Yanga daima mbele nyuma mwiko, kwa hiyo tunaangalia yajayo wala si yaliyopita," alisema Bumbuli.

Kuhusu mechi ya mwisho iliyochezwa Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Yanga ililazimishwa suluhu dhidi ya Dodoma Jiji na kumaliza ligi ikiwa na pointi 74, ikicheza mechi 34, kushinda 21, sare 11.

# SIMBA YAJITABIRIA MAKUBWA KIGOMA

## Manara atamba wanakwenda 'kutegua mitego' huku Gomes...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema siri kubwa ya timu hiyo kuonekana bora kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki msimu huu ni mafanikio yake ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara mara nne mfululizo, Msemaji wao, Haji Manara ametamba wanaenda Kigoma kutwaa ubingwa wa Kombe la FA.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Manara alisema timu yao itaibuka na ushindi wa kishindi katika fainali hizo zitakazochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Manara alisema timu yao haiwezi kufungwa na Yanga kwa mara ya pili mfululizo kwa sababu wamejipanga vyema kuhakikisha wanawadhalilisha watani wao kwa kipigo kikubwa.

"Yanga haiwezi kutufunga kwa mara ya pili, kwa gharama yoyote ile tunaenda kuwadhalilisha kwa kuwafunga idadi kubwa ya mabao na kutetea ubingwa kombe letu la FA, tunajua mtego wao, tutautegua kwa tadhari kubwa, walikopita tunakujua, tutapita huko huko, tunakwenda kushinda kwa kishindo," alitamba Manara.

Naye Gomes aliliambia gazeti hili kikosi cha Simba ni bora ukilinganisha na vikosi vingine ndani ya ukanda huu na hiyo ndio sababu wameshinda idadi kubwa ya mechi pamoja na mabao, lakini wakicheza soka la kuvutia. Kocha huyo ameupongeza uongozi wa klabu hiyo ulioko chini ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mohammed Dewji 'Mo' pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu, Barbara Gonzalez kwa kumwekea mazingira mazuri ya kufanya kazi wakati wote tangu alipotua nchini.

"Huu ubingwa unatoka na kuwa na timu bora kwa sasa hapa Afrika Mashariki, nadhani baada ya muda tutacheza fainali ya Afrika, ukiangalia msimu huu tumefunga mabao mengi na tumeshinda mechi nyingi pia."

"Nikiwa nafikiria kucheza fainali hapo baadaye, ila kwa sasa akili na nguvu zetu tunazielekeza katika mchezo wa Kombe la FA ambao tunakutana na Yanga, dhamira yetu tuchukue Kombe la FA pia kwa kuwafunga Yanga, nina matumaini makubwa ya kufanikisha hilo," alisema Gomes.

Naye Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo, Mwina Kaduguda, alisema sasa wanaelekea Kigoma kuhakikisha wanaibuka na ushindi na Yanga inakwenda katika mashindano ya kimataifa kupitia 'mgongo' wa Simba.

Kaduguda alisema Yanga iliwafunga katika mechi ya ligi kwa sababu 'kuna sehemu' walikosea ila kwa sasa wamejipanga vizuri kuhakikisha wanalipiza kisasi kwa watani zao. "Naenda Kigoma ni nyumbani, yoyote yule shabiki wa Simba ajitokeze uwanjani, Yanga hatoki katika fainali hii, kama wao wanamtegemea huyo mzee Mpili, mimi simfahamu huyo kwa sababu tuna wachezaji wazuri na benchi la ufundi, na tunatarajia makubwa kutoka kwao kuelekea mchezo huo."

"Tuachane na maneno ya vijiweni, mechi yetu dhidi ya Yanga sikuwepo uwanjani, sasa nafunga safari kwenda Kigoma nilipozaliwa, hivyo lazima Yanga apigwe na tuachane na maneno ya huyo mzee wao, kwani malengo yetu ni kuona Yanga anaenda kimataifa kupitia mgongo wa Simba," alisema Kaduguda. Naye winga wa Namungo FC, Shiza Kichuya amesema Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ilikuwa nzuri, bora, yenye msisimko na mvuto wa aina yake.

Kichuya ameipongeza timu yake ya zamani ya Simba kutwaa ubingwa na kusema ilistahili kwa sababu ilijipanga vyema ndani na nje ya uwanja kwa maana kuwa na wachezaji bora, maandalizi pamoja na uwezeshwaji.

"Msimu huu ligi ilikuwa ngumu, nzuri, ilikuwa na ushindani na mvuto mkubwa. Ni moja kati ya ligi bora nilizowahi kucheza. Japo imechelewa kumalizika, lakini ilikuwa na msisimko sana. Tumeona kabisa kwenye ligi hii, timu ambayo huwezi kuitarajia inakwenda kupata matokeo na timu nyingine ambayo haikudhaniwa," alisema Kichuya.

Baada ya mechi yao iliyomalizika kwa kuchapwa mabao 4-0 na mabingwa Simba, winga huyo alibadilishana jezi na Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' huku akisema beki huyo ni rafiki yake tangu wakiwa katika timu ya vijana ya umri chini ya miaka 17.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002